# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*




Uk. 12

## Chadema karibuni kilingeni, ila mjipange!


| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00075 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Julai 24 - 30, 2024 |


MCHANGANYIKO

**DIRA YA TAIFA 2050: 'Kipaumbele ni maendeleo ya viwanda'** Uk. 7



**Mtambue mteja stahiki na unayemlenga** Uk. 8



**Wanasiasa watatu wa upinzani Uganda mbaroni** Uk. 19



**Ni mdahalo ama shambulizi dhidi ya Trump limemng'oa Biden?** Uk. 14



# Rais Dk. Samia kuendelea kujenga nyumba za watumishi wa umma

- **Ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025**

Uk. 4



## NIDA: Rejesheni vitambulisho vilivyofutika maandishi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imewataka wananchi ambao vitambulisho vyao vimepata hitilafu ya kufutika maandishi, kuvirejesha ofisi za NIDA au ofisi za Serikali za Kata, Mitaa, Vijiji na Shehia ambako vitakusanywa... uk. 4

## Maspika Tz, India wapongeza serikali kukuza uchumi, jamii

Uk. 2



**Mtwara** **Wizara ya Fedha yapongezwa kutoa elimu usimamizi wa fedha** Uk. 3

# Kampuni ya gesi lawamani

## ●Mteja adai uzembe wao umemsababishia kuungua mwili wote

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Chamazi Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam, Stanley Nyakunga (40), anailalamikia kampuni moja ya uuzaji wa mitungi ya gesi kwa madai ya kumtelekeza baada ya mtungi wa gesi alionunua kulipuka na kumsababishia majeraha mwilini na hasara ya mali zake.

Alidai kuwa baada ya kuufikisha mtungi huo nyumbani kwake ulivujisha gesi pasipo yeye kugundua.

Alidai baadaye kuwa mtungi huo ulikuwa na kasoro ya kutofungwa kwa lakiri, jambo ambalo alilielezea kuwa ni uzembe.

Nyakunga, alisema wakati amelala yeye na familia yake, usiku alihisi kuwepo kwa harufu isiyo ya kawaida na alipowasha taa ya chemli, mara moto ulilipuka kwenye chumba ambao ulimsababisha majeraha na kuharibu mali zake.

Akizungumza katika ofisi za gazeti la Uelekeo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Nyakunga (pichani), alisema ajali hiyo ilitokea katika nyumba yake iliyopo Chamazi, alfajiri ya Juni 20, mwaka huu.

Alidai kuwa Juni 19, mwaka huu, familia yake ilinunua mtungi wa gesi wa kilo 15 kutoka kampuni hiyo (jina limehifadhiwa kwa muda) katika dukani lililo jirani na makazi yake.

Alisema kwa kuwa kwa wakati huo hawakuwa na matumizi nayo, familia yake ilimsubiri mpaka aliporejea kutoka kwenye shughuli zake ili aunganishe na mfumo wa jiko.

Alidai kuwa, alipoukagua mtungi huo kabla ya kuunganisha na jiko, alibaini kuwa haukufungwa kwa mujibu wa utaratibu wa mitungi ya gesi ambayo hufungwa kwa lakiri kabla ya matumizi.

"Niliuhifadhi ili asubuhi niurejeshe dukani kwa kuwa muda huo (usiku) haukuwa rafiki," alidai Nyakunga na kuongeza:

"Saa 10 alfajiri mvua ikiwa inanyesha, nilihisi harufu kama ya mayai viza (yaliyooza) ndani ya nyumba, nikafungua dirisha ili nijue kama kuna maji machafu yanapita nje, lakini sikuona chochote, na nilipotaka kuwasha taa, umeme ulikuwa umekatika, hivyo nikawasha kibiriti na

ndipo moto wa gesi ulipolipuka kwa kuwa tayari ilikuwa imeshasambaa ndani.

"Nikakumbuka mke wangu na wanangu wawili wamelala chumbani, nikajivuta mpaka ulipo mtungi nikajaribu kuutoa nje huku moto ukiendelea kuwaka, nikavunja mlango mwingine, hapo ndipo mke na watoto wakatoka nje na majirani wakaja kutusaidia kuuzima na kisha kunipeleka hospitali ya Chamazi nikalazwa kwa matibabu," alisema Nyakunga.

Hata hivyo, alisema hospitali ya Chamazi ilimwandikia rufaa kwenda Hospitali ya Temeke, lakini ndugu zake walimhamishia Hospitali Kuu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Lugalo jijini Dar es Salaam.

Alisema alipata nafuu baada ya siku sita na akawapigia simu wahusika wa kampuni hiyo ya gesi Kanda ya Chamazi kuwajulisha kuhusu ajali hiyo.

Aidha, alimtaja mwakilishi wa kampuni hiyo kama Meneja wa Kanda ya Chamazi na alikiri mtungi ulikuwa na kasoro na hivyo akampatia Sh. 500,000 kwa ajili ya matibabu huku akiahidi kumpelekea mtungi mwingine, jiko na vifaa vya kuunganisha mfumo wa jiko, lakini badala yake walimpelekea mtungi bila jiko.

Hata hivyo, alidai kuwa kila anapompigia simu meneja huyo kuhusu majadiliano ya uharibifu uliotokea na afya yake, amekuwa akizungushwa na hajui hatma yake kwa sababu anatumia gharama kubwa kuendelea kujitibu.

"Wamenitelekeza mpaka sasa hawataki kuja tuzungumze kuhusu hatma yangu maana kila baada ya saa tatu, natakiwa kunywa dawa na lita moja ya maziwa," alidai Nyakunga.

Uelekeo ilijamtafuta kwa simu meneja huyo, lakini alituma ujumbe mfupi wa maandishi (sms) kuwa atapiga baadaye.

Na alipopiga simu, alieleza kwamba yeye siyo Msemaji wa kampuni na kuahidi kutoa namba za Msemaji wa kampuni ambaye angezungumzia suala hilo, lakini hakufanya hivyo hadi tunakwenda mitamboni.



---

# Maspika Tz, India wapongeza serikali kukuza uchumi, jamii

**Na Mwandishi Maalum, India**

RAIS wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson na Spika wa Bunge la India (Lok Sabha), Om Birla, wamezipongeza serikali za nchi zao kwa kuimarisha uhusiano wenye kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya nchi hizo.

Walisema hayo wakizungumza katika Ofisi za Bunge hilo jijini New Delhi, India jana.

Spika Dk. Tulia alisema ushirikiano baina ya Tanzania na India umeimarika zaidi baada ya ziara ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan nchini humo mwaka jana.

"Ushirikiano baina ya Serikali zetu umeimarika zaidi baada ya ziara ya Rais Dk. Samia aliyoifanya mwaka jana, ziara hiyo imeongeza wigo wa ushirikiano na ndugu zetu wa India," alisema.

Bunge la India limeahidi kutoa fursa zaidi za mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa umma kupitia Taasisi yake ya Utafiti na Mafunzo ya Kidemokrasia (PRIDE).

Spika Dk. Tulia alisema wajibu wa mabunge hayo ni kushirikiana kwa kuzisimamia na kuzishauri vyema serikali zao kutekeleza mikataba (hiyo) kwa manufaa ya wananchi.

Katika mazungumzo yao pamoja na mambo mengine, Birla alimuelezea Dk. Tulia kuhusu maboresho yaliyofanywa na taasisi hiyo ni pamoja na kuongeza idadi ya ufadhili kwa watumishi wa umma kutoka nchini mbalimbali duniani, hususani, wabunge na watumishi wa mabunge ya nchi hizo.

Pia Birla ametoa kipaumbele mahususi kwa watumishi wa Tanzania kwa kuzingatia urafiki, historia na uhusiano uliodumu kwa muda mrefu baina ya nchi mbili hizo.

Aidha, kwa kutambua pia nafasi ya Dk. Tulia kuwa Rais wa IPU, ameahidi kupitia PRIDE kushirikiana na IPU kuandaa mafunzo kwa watumishi na wabunge wanachama wa umoja huo.



# 'Ole wenu waandamanaji mkiingia eneo linalolindwa'

**NAIROBI, Kenya**

JESHI la Polisi nchini Kenya, limewaonya waandamanaji kutojaribu kuingia katika maeneo yanayolindwa na serikali huku maandamano ya kuipinga serikali yakiendelea.

Onyo hilo lilitoldewa jana Kaimu Inspekta Jenerali wa Polisi, Douglas Kanja Kirocho.

Wakati wa mkutano na waandishi wa habari, Inspekta Kanja asema kuwa ripoti za ujasusi zinaonyesha kuwa maandamano ya sasa yamesheheni vitendo vya fujo vinavyotekelezwa na wahalifu.

"Kulingana na duru za kuaminika, maandamano ya sasa yamegeuzwa kimbilio la wahalifu, walio na ari ya kupora na kuharibu mali ya Wakenya wachapakazi," alisema Inspekta Jenerali Kanja.

Alikuwa akizungumza dhidi ya wito wa vijana wa Kenya kutaka kuingia katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta kupinga utawala wa Ruto.

"Polisi inasisitiza kwamba maeneo yaliyohifadhiwa, hayafai kuingiliwa kama livyoainishwa katika Sheria ya Maeneo yaliotengwa," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Inspekta Jenerali Kanja, maeneo yote yaliyotengwa, ikiwa ni pamoja na mitambo ya LPG na Bitumen na mabohari ya petroli katika eneo la Embakasi, Uwanja wa Ndege wa JKIA, hayapaswi kuingiwa na watu wasioruhusiwa.

Aliongeza kuwa kuwa Sheria ya Usafiri wa Anga ya Kenya inasema ni kinyume cha sheria kuingilia ardhi yoyote ambayo ni sehemu ya uwanja wa ndege wa serikali.

# Wizara ya Fedha yapongezwa kutoa elimu usimamizi wa fedha

**Na Mwandishi Wetu, Mtwara**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala, ameipongeza Wizara ya Fedha kufuatia mpango wake unaolenga kuwapa wananchi uelewa wa masuala ya fedha ikiwemo usimamizi wa fedha binafsi, uwekaji akiba, uwekezaji, kinga za kibima na mikopo iliyo salama.

Alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na wataalamu wa masuala ya fedha kutoka Wizara ya Fedha na taasisi shiriki, waliomtembelea ofisini kwake kwa ajili ya kutambulisha mafunzo hayo yatakayoendeshwa katika wilaya zote za mkoni Mtwara.

"Naipongeza sana Wizara ya Fedha ikishirikiana na taasisi nyingine zikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Benki Kuu, Masoko ya Mitaji na Dhamana na Ofisi ya Rais-Tamisemi, kufika mkoa wetu kutoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha itakayowasaidia wananchi kutumia fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo," alisema na kuongeza:

"Nimeambiwa pia kuwa wananchi watapata elimu inayohusu masuala ya mikopo, nitumie pia nafasi hii kuendelea kuwashauri wananchi wanaohitaji mikopo, kwenda kukopa kwenye taasisi rasmi zilizosajiliwa kisheria kwa usalama wa fedha zao."



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba

Aidha, aliwaasa watoa huduma ndogo za fedha mkoani Mtwara na kwingineko, kuhakikisha wanasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2019 na kuonya kuwa watakaotoa huduma hizo bila kufuata sheria, watawajibishwa kwa mujibu wa sheria tajwa.

Kwa upande wake, Afisa Mkuu Mwandamizi Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Salim Kimaro alieleza kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa kwa wananchi kutokana na wengi wao kuwa na matumizi yasiyo sahihi pale wanapopata fedha.

"Programu hii inalenga kuwafikia wananchi wengi kutoka maeneo mbalimbali, ili pamoja na mambo mengine, wafahamu maeneo rasmi ya kupata huduma za fedha, namna ya kuzisimamia pamoja na kujiwekea utaratibu wa kuweka akiba na kuwekeza kwa ajili ya kupata faida endelevu," alisema.

# Waandamanaji kuelekea Jengo la Bunge mbaroni

**KAMPALA, Uganda**

MAKUMI ya raia wa Uganda wanasemekana kukamatwa na polisi wakati wa makabiliano kati ya maafisa wa polisi na waandamanaji wenye nia ya kuandamana hadi majengo ya Bunge kama ishara ya kupinga ufisadi, kulingana na gazeti la Daily Monitor.

Vijana ambao wamekuwa wakilalamikia ukosefu wa ajira na kupanda kwa gharama ya maisha, walibeba mabango wakimtaka Spika wa Bunge ajuzulu.

Kwa mujibu wa Daily Monitor, Wakili anayetetea haki za kibinadamu, Eriah Nuwenuwe, ni miongoni mwa waliokamatwa katika maeneo ya Bunge.

Tangu juzi, kumeshuhudiwa ulinzi mkali katika maeneo ya majengo ya Bunge na maafisa walijitokeza mitaani kukabili waandamanaji.

Hapo juzi, Kiongozi Mkuu wa Upinzani nchini Uganda, Bobi Wine, alisema vikosi vya usalama katika Mji Mkuu Kampala, vilikuwa vimezingira makao makuu ya chama chake katika mkesha wa maandamano hayo.

Polisi walisema walikuwa wamechukua hatua za tahadhari kuzuia uhamasishaji wa maandamano.

Aidha, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alionya mwishoni mwa wiki kwamba waandamanaji walipopanga kwenda Bungeni, wanacheza na moto. BBC.



# Kesi wizi mil. 19/- 'yapigwa kalenda'

**Hidaya Machupa Na Racheal Mayanga, DARTU**

KESI ya wizi wa Sh. milioni 19.4 inayowakabili Vasant Solanki (73) na Rameshchandra Shah (62), `imepigwa kalenda' baada shahidi aliyepangwa kusikilizwa kupata udhuru.

Hatua hiyo imefikiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Grace Nyarata, akisaidiana na Wakili wa Serikali, Frank Rimoy, ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi, lakini shahidi amepata udhuru wa kuuguliwa na mtoto.

"Mheshimiwa Hakimu, shahidi alikuja mahakamani leo (jana) kwa ajili ya kutoa ushahidi, lakini muda mfupi alipokea taarifa kuwa mtoto wake ni mgonjwa, hivyo, akalazimika kuondoka kwenda kufuatilia matibabu, tunaomba tarehe nyingine ya kusikilizwa," alisema Wakili Nyarata.

Hata hivyo, Wakili wa utetezi, Jamhuri Johnson, aliomba mahakama ifute kesi hiyo kwa madai kuwa upande wa Jamhuri umeshindwa kuita shahidi na washtakiwa wanateseka.

"Kesi hii ilifunguliwa tangu mwaka 2022 na ikafutwa 2023, ikafunguliwa na kufutwa kwa mara nyingine, lakini Aprili 23, mwaka huu, imefunguliwa tena na sababu za miaka yote na shahidi huyo huyo ambaye anatoa sababu mbalimbali kama alivyofanya leo (jana) kutoa sababu za kuuguliwa na mtoto wake, hivyo, ni wazi kwamba kesi hii haiendelei," alisema Wakili Johnson.

Hata hivyo, Wakili Nyarata aliomba mahakama upande wa Jamhuri, upewe nafasi nyingi endapo watashindwa kuleta shahidi basi ombi la utetezi litekelezwe.

Hakimu Lyamuya alikubali ombi la Jamhuri na kumwamuru Wakili wa Serikali kuhakikisha anapeleka shahidi ili kesi iende mbele na haki itendeke.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Agosti 12, mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri na washtakiwa wote wako nje kwa dhamana.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa katika tarehe zisizofahamika kati ya Januari na Novemba, 2016 ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa kwa pamoja walikula njama ya kutenda kosa la wizi.

Katika shitaka la pili, ilidaiwa kuwa tarehe na eneo la tukio la kwanza, washtakiwa kwa pamoja, waliiba Sh. 19,415,000 mali ya Hekalu la Shree Sanatan Dharma Sabh.

# Dk. Samia kuendelea kujenga nyumba za watumishi wa umma

**Flora Bathromew Na Wemael Mmaraba**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, itaendelea kujenga makazi bora kwa ajili ya watumishi.

Alisema hayo katika hafla ya ufunguzi wa jengo la ghorofa saba la makazi ya watumishi wa umma lililopo Magomeni Kota Awamu ya Pili B katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam jana.

Alisema ujenzi wa jengo hilo lililogharimu Sh. bilioni 5.6, ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 na ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia ya kuboresha makazi bora.

Jengo hilo limejengwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

Aidha, Waziri Bashungwa aliwataka wapangaji wanaokaa kwenye nyumba na majengo ya TBA, kulipa kodi ya pango ili fedha hizo zitumike kujenga majengo mapya na kuboresha huduma katika majengo mengine.

"Serikali itaendelea kujenga makazi bora ya watumishi, lakini watumishi mliopata fursa ya kukaa kwenye nyumba za TBA, kulipa kodi ni wajibu.

"Mkilipa kodi, inatupa uwezo wa kuboresha huduma ya makazi bora," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Bashungwa aliielekeza TBA kusimamia ukusanyaji wa madeni kwa wadaiwa sugu kulingana na mikataba waliyojiwekea ili kodi hizo zikamilishe ujenzi wa jengo la tatu na nne (Block C na D) yanayoendelea katika eneo hilo ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 15.

Aidha, alisema serikali imerekebisha Sheria za TBA na kutoa fursa kwa kuingia ubia na sekta binafsi ili kurahisisha ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na taasisi za fedha kwa ajili ya uendelezaji wa milki, kuwahudumia watumishi wa umma wenye uhitaji wa makazi.

Waziri Bashungwa alipongeza TBA kwa matumizi bora ya ardhi na mipango mizuri ya majengo ya kisasa katika eneo la Magomeni lenye ekari 32,000 lililokuwa na wakazi zaidi ya 645 kwa kutumia ekari tisa kutosheleza wakazi hao.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema mkoa huo unatakiwa kupangwa upya kwa kuwa na mikakati ya pamoja kwa kushirikiana na mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuufanya kuwa miongoni mwa miji mikubwa Afrika kufikia mwaka 2030.

Akitoa taarifa ya mradi, Mtendaji Mkuu wa TBA, Msanifu wa Majengo, Daud Kondoro alisema kazi zote katika mradi huo za ubunifu, ujenzi na usimamizi, zimetekelezwa na TBA kwa kutumia wataalam wake kwa kuzingatia mabadiliko chanya ya ukuaji katika sekta ya uchumi, mipango miji na teknolojia ya ujenzi, mawasiliano na miundombinu.

Kondoro alisema jengo hilo limefungwa mfumo wa kisasa wa 'Payless' ambapo itakapofika wakati wa kulipa kodi ya pango na mpangaji akawa hajalipa, moja kwa moja anakosa huduma ya umeme na maji katika nyumba yake na akilipa kodi ya pango, muda huo huo huduma ya umeme na maji inarejea.



**Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa (wa tatu kutoka kulia), akikata utepe wakati wa ufunguzi wa jengo la pili Magomeni Kota jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kutoka kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila na kushoto kwake ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daud Kondoro.**

# NIDA: Rejesheni vitambulisho vyote vilivyofutika maandishi

**Na Mwandishi Wetu**




MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imewataka wananchi ambao vitambulisho vyao vimepata hitilafu ya kufutika maandishi, kuvirejesha ofisi za NIDA au ofisi za Serikali za Kata, Mitaa, Vijiji na Shehia ambako vitakusanywa na kwa ajili ya kuchapishwa upya.

Mkurugenzi wa Idara ya Vitambulisho kutoka NIDA, Edson Guyai, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wamepokea taarifa ya kuwepo kwa vitambulisho vichache kufutika taarifa zailizochapwa mbele au nyuma ya kitambulisho, mfano majina, picha au namba ya kitambulisho au tarehe ya kuzaliwa.

Alisema takwimu za NIDA zinaonyesha kuwa vitambulisho vyenye hitilafu hiyo ni 21,224 sawa na asilimia 0.09 ya vitambulisho 21,32,098 vilivyotengenezwa.

"Mwananchi ambaye kitambulisho chake kina changamoto hiyo, akirudishe ofisi ya NIDA au kwa mtendaji alipokichukua ili virudishwe na kuchapishwa upya," alisema.

Alisema kumekuwa na upotoshaji kuhusu ubora wa Vitambulisho vya Taifa kutokana na changamoto hiyo ndogo iliyojitokeza na alisisitiza kwamba vitambulisho vinavyotolewa na NIDA, vina ubora unaokidhi viwango vya kimataifa.

Hata hivyo, alisema kwa sasa wataalamu wanaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha tatizo hilo kama ni mashine, wino au kadi.

"Hii itawezesha kufidiwa kwa kadi hizo kama yalivyo matakwa ya mkataba bila serikali kuingia gharama yoyote," alifafanua.

Alisema hitilafu ndogo ndogo, ni jambo la kawaida kutokea katika sekta ya uzalishaji wa bidhaa duniani huku akieleza kuwa hata kampuni kubwa za uzalishaji kama wa magari na simu za mkononi, hupata changamoto kama hizo.

# NEMC yamtunuku Tuzo Jafo, awaaga watumishi akiwamwagia sifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, ameagana na watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) huku akipewa ?Tuzo ya kutambua mchango wake katika masuala ya mazingira.

Hafla hiyo inafuatia mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Dk. Samia Suluhu Hassan ambapo Waziri Jafo aliteuliwa kuiongoza wizara hiyo akitoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Kwa sasa; Dk. Ashatu Kijaji, ndiye Waziri wa ofisi hiyo.

Akizingumza wakati wa hafla ya kuagana na wayumishi hao jijini Dar Salaam, Waziri Jafo aliwashukuru watumishi wote wa MEMC kwa kutoa ushirikiano kipindi chote alichokuwa akihudumia kwa nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ikiwa ni pamoja na kazi nzuri wanaoyoifanya ya kusimamia uhifadhi wa mazingira na miradi zaidi ya 9,000 inayolenga kuleta maendeleo nchini.

"Ndugu zangu, niwapongeze na ninajivunia kufanya kazi nanyi kwa kipindi chote nilichokuwa hapa, uwekezaji wa miradi karibu 9,000, imesajiliwa na huu ni uwekezaji mkubwa sana na mikono yenu ndiyo inashughulikia miradi hiyo. Niwapongeze kwa kusimamia miradi hii kwa kasi kubwa na kutekeleza majukumu yenu," alisema Waziri Jafo.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) baada ya kukabidhiwa Tuzo ya kutambua mchango wake kwenye masuala ya mazingira alipokuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Pia alitoa wito kwa watumishi kushirikiana na Waziri Kijaji katika utekelezaji wa majukumu ya serikali hasa masuala yote ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dk. Immaculate Sware Semesi?,?alimpongeza Waziri Jafo kwa kazi kubwa aliyoifanya ikiwa ni pamoja na kusimamia miradi inayolenga kutunza mazingira kama mradi wa kudhibiti matumizi ya zebaki, kusimamia utekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki na sauti zilizozidi viwango.




# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

**HII NI KERO**

## Trafiki wanapogeuka roboti -1

Ni kweli, taratibu na sheria zinataka magari yasiyosajiliwa kama ya kubeba abiria yasibebe abiria. Lakini kuna nyakati za jioni au asubuhi katika Jiji kama la Dar es Salaam usafiri unakuwa mgumu sana, lakini gari ndogo zikisimama kwenye vituo vya daladala kusanya na kusaidia wananchi usafiri zinakamatwa kwa kuwa hazijasajiliwa kwa ajili hiyo.

Sheria au kanuni hii inapaswa kuangaliwa upya kwa sababu haina tija na inaongeza ugumu wa maisha bila sababu. Kibaya zaidi askari wa usalama barabani wanaitumia hii kuwapiga bao wenye kutaka kusaidia abiria na kuvuna pesa wao. Yaani wakati wanaona hali ya usafiri ilivyo mbaya bado wanazuia magari madogo kusaidia abiria kuwahi kazini au majumbani. Huku ni kufanya kazi mithili ya roboti.




**MAONI YA MHARIRI**

# Wanaoeneza hofu katika jamii washughulikiwe

Katika siku za karibuni, wazazi, hususani wa Dar es Salaam walikumbwa na hofu kubwa juu ya watoto wao kutokana na taarifa za uwepo wa watu wanaoteka nyara watoto kisha kuwaua na kunyofoa baadhi ya viungo.

Tukio la karibuni lilijiri juzi Julai 22, ambapo taarifa zilienea mitandaoni zikidai kwamba watoto wawili wa Shule ya Msingi Brayson iliyopo Mburahati, Ubungo, wametekwa nyara na gari aina ya Noah yenye rangi nyeusi ambayo haikuwa na namba za usajili.

Taarifa hiyo ilikuja baada ya kuwepo kwa mlolongo wa taarifa za utekaji nyara wa watoto kama iliyohusisha Shule ya Msingi Kisewe iliyoko Mbagala, ikidaiwa kwamba wanafunzi shuleni hapo waliuawa, wakatolewa figo na kunyofolewa macho.

Taarifa nyingine iliyosambaa kupitia mitandao ya kijamii ilihusu watoto wanne wa Kigamboni wakidaiwa kuuawa na kuwekwa kwenye viroba.

Nyingine ilihusu Shule ya Sekondari Majani ya Chai iliyoko Kipawa kwamba eti kuna wanafunzi watatu wa shule hiyo wamuawa na watu wasiojulikana.

Habari hizo ambazo majina ya watoto waliouawa au kutekwa nyara yalikuwa hayatajwi zilikolezwa na uwepo wa tukio la kweli lililojiri Goba jijini humo.

Hilo lilihusisha dada wa kazi za nyumbani, Clemensia Mirembe (19), kumjeruhi mtoto wa mwajiri wake ikidaiwa kumkata na kitu chenye ncha kali shingoni. Msichana huyo ameshakamatwa.

Baada ya uchunguzi wa matukio hayo, Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limesema kwamba ukiondoa tukio la Goba, mengine yaliyobaki ni ya uongo yaliyolenga kuzua taharuki kwa wananchi.

Katika taarifa kwa umma usiku wa kuamkia jana, Kamanda wa Kanda hiyo, SACP Jumanne Muliro, amesema wamefuatilia kwa kina habari hizo na kugundua bila kuacha mashaka kwamba zimepikwa na watu waliolenga kuzua taharuki katika jamii.

Kamanda Muliro amesema tayari mtu mmoja aliyezusha tukio la Mbagala anashikiliwa na polisi huku wengine au watu anaoshirikiana naye kufanya uzushi huo wakisakwa.

Tunalipongeza Jeshi la Polisi kwa kugundua haraka kwamba matukio haya yanatengenezwa na watu ili kueneza hofu kwa wananchi kwa sababu wanazozijua wao.

Uchunguzi wetu umeonesha kwamba taarifa hizi za uzushi zilisababisha hofu kubwa miongoni mwa wazazi, baadhi wakawa wanaacha shughuli zao ili kusindikiza watoto wao shuleni na kwenda kuwapokea baada ya muda wa masomo.

Katika tukio moja Temeke juzi, bajaji moja ilipita kisha kikasikika kilio cha mtoto, hali iliyozua taharuki na kusababisha watu kukodi pikipiki na silaha za jadi kuifukuza hiyo bajaji, kumbe alikuwa ni mama akinyonyesha mtoto aliyekuwa akilia kawaida tu.

Kama uungwana usingetumika, amani ingevunjika.

Tunawaomba polisi kuhakikisha wote waliohusika na uzushi huu wanakamatwa na kuadhibiwa kwa vyombo vya sheria kwa mujibu wa sheria zetu.

Kwa upande wa wananchi tunawasihi kuacha 'kushea' taarifa za kwenye mitandao ambazo chanzo chake hakijulikani na wala hazijathibitishwa na mamlaka husika kuhusu usahihi wake.

Tunawasihi pia kuendelea kushirikiana na Jeshi lao la Polisi katika kuhakikisha watoto wanaendelea na masomo bila hofu.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |


Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

# Tujitenge na ushirikina Watanzania

JUMAMOSI iliyopita, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye anajulikana kama Chifu Hangaya alikutana na machifu wenzake kule Ikulu ya Chamwino Dodoma, ambako pamoja na mambo mengine alikemea vikali mauaji yanayoendelea sehemu mbalimbali nchini kwa watoto wadogo na maalbino.

Dk. Samia alisema vitendo vinavyoendelea kukithiri vya utekaji wa watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi (maalbino) kisha kuwaua na kunyofolewa viungo vya miili yao, havikubaliki na hivyo ameagiza kila Mtanzania kushiriki katika kutokomeza tabia hizi chafu za kishirikina.

Amewataka machifu waliohudhuria kikao hicho kutoka Tanzania nzima kuwa sehemu ya viongozi wa kupiga vita janga hili la kifedhuli kwa kukemea na kuwaelimisha watu wao juu ya kadhia hii kwa taifa letu.

"Kila kitu mnaiachia Serikali Kuu, wakati ninyi ndiyo mpo karibu na watu wanaofanya vitendo hivi vya mauaji, kuanzia sasa nendeni mkashirikiane na viongozi wa ngazi ya chini wa Serikali, viongozi wa dini na mila kuhakikisha ujinga huu unakoma," ameagiza Dk. Samia.

Amewataka viongozi wa ngazi ya chini kuacha kufumbia macho vitendo hivi, kwani mauaji yakitokea lawama zote zinakwenda kwa Serikali Kuu na vyombo vyake vya dola wakati wao ndiyo wapo karibu na wahalifu hao.

Inasikitisha, sijui ni nani aliyeturoga Watanzania! Ushirikina umekuwa sehemu ya maisha yetu, ni aibu kubwa kuendekeza ushirikina katika karne hii mapinduzi ya nne ya viwanda yenye matumizi ya akili mnemba!

Yalianza mauaji ya vikongwe kule Kanda ya Ziwa wakituhumiwa ni wachawi, kisa macho mekundu yanayotokana na kuchochea kuni za kupikia chakula katika sehemu kubwa ya maisha yao. Zikapigwa kelele kubwa siku hizi mauaji ya wazee yametulia.

Likaibuka la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na kunyofolewa viungo vyao huko hukohuko Kanda ya Ziwa lililokwenda sambamba na mauaji ya watu kule Kanda ya Nyanda za Juu hususani mkoani Mbeya na kuchunwa ngozi!

> **Kila kitu mnaiachia Serikali Kuu, wakati ninyi ndiyo mpo karibu na watu wanaofanya vitendo hivi vya mauaji, kuanzia sasa nendeni mkashirikiane na viongozi wa ngazi ya chini wa Serikali, viongozi wa dini na mila kuhakikisha ujinga huu unakoma**

Zikapigwa tena kelele mauaji hayo yakatulia. Kuna wakati yaliibuka mauaji ya watu wenye vipara (ualaza) lakini nayo yametulia.

Sasa yameibuka upya mauaji kwa ajili ya viungo karibu nchi nzima na safari hii si tu albino ndiyo walengwa wakuu, bali hata watoto wadogo wasio na ulemavu wowote wamegeuka kuwa wahanga wa mauaji haya ya kutisha na kikatili.

Haya ni matokeo ya jamii zetu kuendelea kukumbatia Imani za hivyo na kuamini waganga badala ya kuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Hali hii ya mauaji inacha makovu katika jamii kwa kuchukiana, kuwindana kwa visasi na kuondoa sifa kubwa tuliyojenga kwa miaka mingi kwamba taifa letu ni la amani na utulivu!

Tuungane na Rais Dk. Samia kukemea, kupiga vita, kulaani kwa vitendo vya kuwataja na kuwakamata washirikiana hawa. Wanatuharibia sifa nzuri ya amani ya taifa tuliyoitunza kwa miaka mingi sana.

## DIRA YA TAIFA 2050:

# ‘Kipaumbele ni maendeleo ya viwanda’

**Na Mwandishi Wetu**

MAANDALIZI ya Dira ya Taifa 2050, imeweka kipaumbele kikubwa kwenye maendeleo ya viwanda nia ikiwa ni kuondoa utegemezi wa kununua bidhaa nyingi nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wadau wa viwanda jijini Dar es Salaam jana.

Mkutano huo ulioandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), pia ulizindua tuzo za Rais za Mzalishaji Bora Viwandani PMAYA ambazo hufanyika kila mwaka kwa wenye viwanda.

Profesa Mkumbo alisema wasomi mbalimbali wamesema kwenye maandiko yao kuwa tofauti kubwa baina ya nchi tajiri na zile maskini, ni kwamba nchi tajiri zina viwanda vingi wakati nchi maskini hazina viwanda na zinategemea kununua bidhaa nje ya nchi.

“Itakuwa vigumu sana kutengeneza Dira ya Taifa bila kuweka viwanda katikati ya dira hiyo kwa sababu hilo ni la msingi na tafiti nyingi zinaonyesha kuwa hatuwezi kuendelea kwa kuendelea kununua bidhaa nje ya nchi, lazima tuwe na viwanda vingi tuuze nje,” alisema.

Alisema utafiti uliofanywa na serikali katika maandalizi ya dira hiyo uliohusisha watu 7,668 nchi nzima waliochaguliwa kisayansi, walitaka vipaumbele vitano viwepo kwenye dira hiyo.

Moja ya kipaumbele kilichotajwa na wananchi hao ni suala la viwanda na kwamba asilimia 65 ya malighafi zinazotumika viwandani, zinatokana na kilimo, hivyo kilimo nacho kitaendelea kuwa kipaumbele kwenye dira hiyo.

Alisema kipaumbele kingine kilichotajwa kwenye utafiti huo ni uwekezaji mkubwa kwenye rasilimali watu kwani uchumi wa viwanda unahitaji watu waliosoma vizuri.

“Lazima dira yetu ituelekeze kuwekeza kwenye elimu na siyo elimu tu bali elimu iliyo bora,” alisema Profesa Mkumbo.

Naye Mwenyekiti wa CTI, Leodegar Tenga, alisema wadau wa viwanda wamekutana kujadili Dira ya 2050 na kuzungumzia maendeleo ya viwanda kwa ujumla ili kuhakikisha hayasahauliki kwenye dira hiyo.

“Tunashukuru Waziri amezungumza kwamba bila viwanda, hakuna maendeleo na ametoa mifano ya nchi nyingi zilizoendelea namna zilivyopiga hatua kwenye viwanda,” alisema Tenga.

“Hakuna nchi duniani hata moja ambayo iliwahi kupiga hatua kubwa kiuchumi bila kuwekeza kwenye viwanda, kwa hiyo lazima tuwe na mikakati madhubutu na kuna msemo wa Kiswahili kwamba kupanga ni kuchagua kwa hiyo tuchague kuwekeza kwenye viwanda ili tusonge mbele,” alisema.

Aliongeza kuwa ili viwanda vifanye kazi vizuri, lazima serikali iwekeze pia kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara na reli na kuwekeza kwenye rasilimali watu.

“Maono ya nchi ni kujipanga ili tutimize tulichopanga kwa hiyo sisi CTI tunaamini viwanda ni muhimu na ili kupata rasilimali, lazima tuwe na kilimo kwa hiyo lazima tuwekeze pia kwenye kilimo,” alisema.

“Tumefungua masoko mengi upande wa Afrika Mashariki (EAC), Kusini mwa Jangwa la Sahara sasa tujipange kuuza bidhaa zetu za viwanda nje ya nchi badala ya sisi kuwa soko la bidhaa za wenzetu,” aliongeza Tenga.

Makamu Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, alisema nchi inapaswa kuwa na viwezeshaji vinavyofaa kama teknolojia, rasilimali watu na miundombinu.

“Zaidi ya hayo, ni lazima tujenge msingi imara wa amani, utulivu, umoja, kujitegemea, na muundo wa utawala unaoongoza mkono uwajibikaji, uwazi na kufanya maamuzi shirikishi,” alisema.



## Shahidi: Mshtakiwa aliniomba nisaidie kutafuta mnunuzi wa gari

**Na Racheal Mayanga, DARTU**

SHAHIDI Ahmed Malungu (54), fundi magari katika kesi ya wizi wa gari inayomkabili Ally Musa (33), amedai mahakamani kukutana na mshtakiwa kibanda cha Tigopesa aliyedai kuwa anauza gari yake aina ya RAV4.

Alitoa ushahidi huo juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalo, dhidi ya mshtakiwa.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa kati ya Oktoba 24 na Desemba 2, 2021 Mtaa wa Bukoba, wilayani Temeke Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa aliiba gari aina ya Toyota RAV4 lenye namba za usajili T 933 DQA yenye thamani ya Sh. milioni 16.7 mali ya Lucas Shinze.

Shinze alilipeleka gari hilo gereji anayofanyia kazi mshtakiwa kwa ajili ya matengenezo, lakini mshtakiwa hakufanya hivyo.

Alidai kuwa Novemba, 2021 alijulishwa na mshtakiwa kwamba anauza gari lake aina ya Toyota RAV 4, hivyo, akaombwa amtafutie mnunuzi.

“Nilimuunganisha kwa rafiki yangu Dogras (alimtaja kwa jina moja), lakini Dogras pia alikuwa na rafiki yake, ambaye ndiye alikuwa akilihitaji hivyo, alimpa Dogras namba ya Ally na kilichoendelea sikufahamu,” alidai.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Agosti 19, mwaka huu, itakapoendelea kwa ushahidi mwingine.

# `Taasisi zingatieni tathmini ya mazingira kabla ya mradi’

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limezitaka taasisi za serikali na binafsi, kuzingatia umuhimu wa ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya mradi kuanza ili kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii kutoka NEMC, Lilian Lukambuzi, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana.

Mkurugenzi huyo alikuwa akikabidhi cheti cha tathmini hiyo kwa mratibu wa mradi wa kudhibiti matumizi ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu kufuatia ujenzi wa kituo cha kutoa elimu ya udhibiti wa matumizi ya zebaki kinachotarajiwa kujengwa mkoani Geita.

Alisema TAM ndiyo msingi pekee utakaotoa nafasi ya kutambua athari za kimazingira katika eneo husika na kutoa nafasi ya kuendeleza mradi wowote na kuzingatia udhibiti wa mazingira.

“Sisi kama NEMC, ndiyo waratibu wa mradi wa kudhibiti matumizi ya kemikali ya zebaki, hivyo ni lazima tuwe mstari wa mbele kutekeleza masuala ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake hasa ya ufanyaji wa Tathmnini ya Athari za Mazingira kwenye utekelezaji wa miradi kabla ya kuanza ili kutunza mazingira,” alisema.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Kemikali ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Mhandisi Dk. Befrina Igulu, alisema mradi huo unatekelezwa katika Mikoa ya Geita, Shinyanga, Mara, Singida, Mwanza, Mbeya na Songwe, hivyo ni muhimu kuwa na kituo kwa ajili ya mafunzo.

Alisema kituo hicho kimezingatia matakwa yote ya kimazingira na kimekidhi vigezo vya Tathmnini ya Athari kwa Mazingira na kitakuwa na miundombinu wezeshi ya utunzaji wa mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Alisema elimu ya matumizi salama ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu inatakiwa kizingatiwa, hivyo uwepo wa kituo hicho kutasaidia wachimbaji kwa makundi kupatiwa elimu ya matumizi salama ya zebaki.



**Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Jamii wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Lilian Lukambuzi, akimkabidhi cheti Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Sware Semesi cha TAM cha mradi wa kituo cha elimu ya kudhibiti matumizi ya kemikali ya zebaki kitakachojengwa Geita.**



Na Ahmed Rage Simu: 0717 658574

# Mtambue mteja stahiki na unayemlenga

KATIKA ulimwengu wa biashara, kuelewa na kutambua mteja stahiki na anayelengwa, ni jambo la msingi kwa mafanikio ya biashara.

Hii ina maana ya kufahamu ni nani anayehitaji bidhaa au huduma yako na jinsi ya kuwafikia kwa ufanisi.

Njia bora za kutathmini soko, zinaweza kusaidia biashara kutengeneza mikakati madhubuti, kuongeza mapato, na kuboresha uhusiano na wateja.

Kupitia makala hii, tutachambua hatua muhimu na mbinu bora za kutambua na kuelewa soko lako.

**1. UTAFITI WA SOKO**

Utafiti wa soko ni hatua ya kwanza na muhimu katika mchakato wa kutambua mteja stahiki.

Hii inajumuisha kukusanya na kuchambua taarifa kuhusu soko lako, washindani na wateja wako.

**a. Utafiti wa Awali**

Huu ni utafiti ambao unakusanya taarifa moja kwa moja kutoka kwenye chanzo chake.

Kuna njia kadhaa zinazoweza kutumika ili kufanikisha hili. Miongoni mwao ni kama nitakavyoorodhesha hapo chini.

**Mahojiano:** Kuongea na wateja wa sasa na watarajiwa ili kuelewa mahitaji yao, maoni

yao kuhusu bidhaa/huduma yako na matarajio yao. Mahojiano yanaweza kufanywa ana kwa ana, kwa simu au kwa njia ya mtandao.

**Utafiti wa maswali:**

Kusambaza maswali kupitia barua pepe, mitandao ya kijamii, au dodoso ili kupata maoni ya wateja wengi kwa haraka. Utafiti huu unaweza kuwa na maswali yanayohitaji jibu la ndiyo au la ama yanayohitaji majibu ya kutoa maelezo.

**Vikao vya majadiliano:**

Kukusanya kundi la watu ambao wanafanana na wateja wako stahiki ili kujadili na kupata maoni yao kuhusu bidhaa au huduma yako.

Hii inasaidia kupata ufahamu wa kina kuhusu mitazamo na hisia za wateja.

**b. Utafiti wa ziada**

Huu ni utafiti ambao unakusanya taarifa zilizopo tayari kutoka vyanzo mbalimbali kama vile ripoti za soko, tafiti zilizofanywa na mashirika mengine, na makala za kitaalamu.

Utafiti wa ziada unaweza kutoa mwanga kuhusu mwenendo wa soko, tabia za wateja, na mikakati ya washindani.

**2. UCHAMBUZI WA TABIA ZA WATEJA KUELEWA TABIA NA MIENENDO YA WATEJA, NI MUHIMU KWA KUTAMBUA MTEJA STAHIKI.**

Hii inaweza kufanywa kupitia zana za kitaalamu zaidi.

**a. Uchambuzi wa takwimu (Data Analysis)**

Kwa kutumia zana za kisasa za uchambuzi wa takwimu, unaweza kuchambua data kutoka kwa tovuti yako, mitandao ya kijamii, na mifumo ya uuzaji ili kuelewa tabia za wateja wako.

Hii inajumuisha kujua ni bidhaa gani zinauzwa zaidi, muda gani wateja hutumia kwenye tovuti yako na jinsi wanavyoingiliana na chapa yako mtandaoni.

Uchambuzi wa takwimu unaweza kusaidia kubaini fursa za soko na maeneo yanayohitaji kuboreshwa.

**b. Uchambuzi wa tabia za ununuzikufuatilia jinsi wateja wanavyonunua bidhaa au huduma yako.**

Hii inaweza kujumuisha njia wanazotumia kufanya ununuzi, mzunguko wa ununuzi na bidhaa wanazopendelea zaidi.

Kwa mfano, unaweza kuchambua data za mauzo ili kubaini bidhaa zinazouzwa zaidi katika vipindi tofauti vya mwaka au maeneo tofauti.

**3. UTAMBUZI WA SOKO LENGWA**

Baada ya kukusanya na kuchambua taarifa, hatua inayofuata ni kutambua soko lengwa.

Hii inahusisha kugawanya soko kubwa kuwa sehemu ndogo ambazo zina sifa

zinazofanana. Njia bora ni kupitia njia mbili kuu.

**a. Soko Kitasnia**

Kugawanya soko kulingana na sekta maalum, kama vile afya, elimu, au teknolojia.

Hii inaruhusu biashara kuunda ujumbe maalum unaolenga sekta hizo kwa usahihi zaidi.

Kwa mfano, kampuni inayouza vifaa vya matibabu inaweza kulenga hospitali na vituo vya afya kama soko lake kuu.

**b. Soko Kidemografia**

Kugawanya soko kulingana na vipengele vya demografia kama vile umri, jinsia, kipato au eneo. Hii inasaidia kuelewa mahitaji ya vikundi tofauti vya watu na jinsi ya kuwasiliana nao kwa njia inayofaa. Kwa mfano, bidhaa za urembo zinaweza kulengwa kwa wanawake wenye umri wa kati ya miaka 18 na 35 wanaoishi mijini.

**4. UUNDAJI WA SIFA ZA MTEJA STAHIKI**

Mteja stahiki ni mwakilishi wa mteja wa kawaida anayelengwa.

Uundaji wa sifa za mteja stahiki, unasaidia biashara kuelewa vizuri zaidi mahitaji, tabia, na changamoto za wateja wao.

**Hatua hii inahusisha:-**

Kuanisha Tabia za mteja stahiki: Kuelezea mteja wako wa kawaida kwa kutumia

data halisi kama umri, jinsia, kazi na mapendeleo ya binafsi. Hii inajumuisha taarifa kama vile jinsi wanavyotumia bidhaa zako, vyanzo vya habari wanavyopendelea, na mitazamo yao kuhusu chapa yako.

**Itaendelea....**



*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Julai 24 - 30, 2024




# Chadema karibuni kilingeni, ila mjipange!

Jarida hili haliuzwi

UK. 12 & 13




UK. 10

UK. 15



# Malipo kielekitroniki yanapaisha mapato lakini tujizatiti

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Tanzania imejaaliwa kuwa na ardhi nzuri na ya kutosha inayoweza kuzalisha mazao kibiashara na chakula kingi. Watanzania tunatakiwa kumshukuru Mungu kwa zawadi ya ardhi yetu na pia kutujalia kuishi kwa amani na utulivu.

Kimsingi ni kwa neema ya Mungu tumejikuta tunaishi hivyo, inatupasa kumshukuru na kumtukuza maana ni yeye anayetustahilisha kuitwa Watanzania.

Zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wote wanaelezwa kwamba wanaishi kwa kutegemea kilimo na hapo hujaweka wanaotegemea ardhi yetu kama wafugaji, wachimba madini, walioko kwenye sekta ya utalii na kadhalika na kadhalika.

Shughuli mbalimbali zinafanywa kwenye ardhi na wananchi na wawekezaji, ambapo mbali ya wao wenyewe kujipatia kipato lakini pia ni chanzo cha mapato kwa Serikali.

Tanzania tulimaliza mwaka wa fedha 2023/2024 ambao Bunge lilipitisha matumizi ya Serikali ya shilingi trilioni 44.4. Hivyo, Julai Mosi, 2024, tukaanza rasimi mwaka mwingine wa fedha baada ya Bunge kupitisha shilingi trilioni 49.35 zitakazotumika hadi Juni 30, 2025. Hivyo, Serikali inatarajia kutumia rasilimali fedha nyingi zaidi ukilinganisha na miaka iliyopita. Hiki ni kiasi kingi cha fedha na hivyo wananchi tunatarajia mengi yatakayotekelezwa na serikali yetu hadi Juni 30, 2025.

Pamoja na ongezeko la bajeti ya 2024/2025, bado ni mipango tarajiwa; utekelezaji rasmi utategemea ukusanywaji wa kodi na mapato mengine ya Serikali. Wizara ya Fedha (HAZINA), ndiyo chombo mahususi kinachosimamia masuala ya mapato na matumizi ya fedha za Serikali kwa kushirikiana na vyombo vingine hususani Benki Kuu, taasisi zinazohusika na ukusanyaji wa fedha hususani TRA, serikali za mitaa na taasisi za umma.

Bunge pia kupitia kamati zake za kisekta, huwajibika kufuatilia matumizi ili yaendane na kilichopitishwa na Bunge. Vilevile, hupitisha muswada ambao ukisainiwa na Rais, huwa Sheria ya Fedha ili makadirio na matumizi ya fedha yapate nguvu ya kisheria.

Hata hivyo, makadirio na matumizi ya fedha za umma huendana na mipango ya kitaifa ya muda mfupi na mrefu. Vilevile panakuwepo na miongozo mbalimbali ili kuweza kusimamia utekelezaji na hatimaye kufanikisha kile kilichokusudiwa kwa faida ya Watanzania wote.

Kwa kuwa nia ya makala haya ni kusisitiza matumizi ya mifumo ya kielekitroniki katika kukusanya na kuimarisha hazina ya serikali; ilibidi kupitia bajeti ya mwaka wa fedha uliopita (2023/2024) ili kubaini nini kilijiri kuhusiana na matumizi ya kielekitroniki kufanikisha makusanyo kupitia mialama husika.

Kimsingi, pamoja na mambo mengine, Serikali ilisisitiza na kuweka mkazo juu ya matumizi ya mifumo ya kielekitroniki.

Mathalani, pamoja na mengineyo mkazo wa Serikali ulilenga yafuatayo: (i) kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliono (TEHAMA) katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali (ii) Kuendeleza kuhimiza matumizi ya mfumo wa Serikali wa Kielekitroniki wa malipo ya Serikali (GePG) kwa Wizara na taasisi nyingine za Serikali na kuhakikisha matumizi ya namba ya udhibiti katika miamala yote ya Serikali na (iii) Kuhakikisha matumizi zaidi ya kielekitroniki kwa kutumia kifaa cha kukusanya fedha (EFD) ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi na tozo mbalimbali.

Hiyo ni mifano michache ya kielekitroniki kwenye ulimwengu wa kidijitali; ambayo katika uhalisia wake ikitumiwa vizuri inaweza kupaisha mapato ya Serikali kwa kiasi cha kutosheleza mahitaji ya taifa kila mwaka bila kuhangaika kukopa.

Hata kama tukilazimika kukopa iwe ni kwa kiasi kidogo tu. Swali la kujiuliza ni: je, tunakopa kila mwaka ili kufanya kitu gani cha lazima?

Iwapo nia ni kutaka Watanzania waende kwenye mwezi, wengi tutasema hilo siyo hitaji la msingi kulazimika kukopa? Lakini vipaumbele vya taifa vikiwa vyenye kuinua maisha ya waliowengi nchini, tunaweza tukakopa iwapo nguvu zetu zimepwaya na pawepo sababu za kuridhisha.

*Inaendelea uk. 18*



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Chadema haina mwelekeo, haina watu wa kuongoza nchi



Mch. Peter Msigwa

HEBU jaalia kikatokea cha kutokea, Watanzania wakalewa cha kulewa na kukikabidhi nchi Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), unadhani chama hicho kina watu madhubuti wa kuunda Baraza la Mawaziri ili kusimamia sera zao?

Jambo hili nilikuwa sijalitilia maanani sana lakini wiki iliyopita, kada wa zamani wa Chadema ambaye ametimkia CCM, Mchungaji Peter Msigwa alinizindua na kuona ukweli kwamba chama kile hakina safu ya viongozi unaoweza kusema wataweza kuunda serikali kama utawakabidhi nchi leo.

Mbaya zaidi, licha ya kupoteza watu muhimu kila kukicha huoni chama hicho kikiwa na mikakati ya kuvutia watu makini kujiunga nacho ukiacha kile ambacho Mchungaji Msigwa anasema kimekalia kuwapa vijana wachache wanaojiunga nacho matumaini feki!

Chadema ya leo si ile ya mwaka 2010 wakati ilipomsimamisha Dkt. Wilbrod Slaa kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano kwa maana ya kuwa na wanasiasa wengi imara na makini ambao wengi wameshakihama chama hicho, asilimia kubwa wakirejea chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wachache wakienda vyama vingine.

Na bila shaka, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan siku hizi za kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na baadaye mwaka kesho Uchaguzi Mkuu, tutashuhudia wengi wakizidi kukikimbia chama hicho kuanzia kwenye serikali za mitaa, udiwani hadi ubunge.

Katika moja ya mikutano ya CCM ambayo Msigwa ameshiriki huku akijaribu kueleza kilichomkimbiza kutoka Chadema ni kushtukia kwamba Chadema haina tena wanasiasa wa maana ambao unaweza kusema wanaweza kuunda baraza imara la mawaziri kama leo utawakabidhi nchi.

"Nikienda Kenya. Nikiangalia vyombo vya Habari Kenya. Nikiangalia Raila Odinga line-up yake, unamkuta hapa kuna Raila mwenyewe, kuna Martha Karua, James Orengo, kuna Kalonzo Musyoka, Moses Wetangula, kuna Sakaya na wengine lukuki. Hata wakisimama kwenye televisheni kwamba hii ni serikali mbadala ya Odinga walau Wakenya wanamwelewa," anasema.

Anasema hata ukienda Afrika Kusini, chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) cha Julius Malema ambacho hakina muda mrefu tayari kina wanasiasa wengi machachari ambao ukiwakabidhi nchi hata leo kuna watu utawatumainia kuendesha wizara achilia mbali kuwa wakuu wa mikoa wenye itikadi sahihi ya chama na kuwa tayari kubeba na kutekeleza sawia sera za chama.

Maneno haya yana mantiki sana kwa sababu si kila mmoja wetu anaweza kuongoza wizara au mkoa, achilia mbali kuongoza wilaya na nafasi nyingine za uteuzi. Hapo juu nimegusia kwamba ukilinganisha Chadema ya 2010 na hii ya sasa mintarafu suala zima la kuwa na wanasiasa wenye uwezo, ni sawa na kulinganisha mbingu na ardhi!

Ndio maana Msigwa anasema: Nikamwambia Nkrunzinza (Freeman Mbowe), kwamba hivi Watanzania tuchukulie wameikataa serikali ya Chama Cha Mapinduzi, hivi kwenye kambi yako hapa Waziri Mkuu ni nani? Waziri wa Kilimo (makini) kama Bashe (Hussein) ni nani? Waziri wa viwanda unampata pale Chadema? Sasa kwa nini tunataka Watanzania watuamini wakati line-up yenyewe ni mgogoro?

"Kwa sababu mimi ninapenda mijadala yenye tija. Nikamwambia Nkrunzinza kwambia kwa muda wa miaka saba chama kimeshindwa kuvutia vijana wenye maono. Huwezi kupata vijana wa generation Z ndani ya chama chetu ambao wana challenges zao, kwani watu wenye akili wote chama kina wa- expel (kinawaondoa)... Ukienda kwa akina mama huwezi kupata wanawake makini ambao wakikaa pale wanavutia wengine. Huwezi kupata," anasema.

Anachosema Mchungaji kinaonekana ni kweli kwani takribani kila mwaka, kama si kila siku, Chadema inakimbiwa na watu kuanzia chini kwenye ngazi ya uwenyekiti wa kijiji na kuendelea. Kwa mfano, mwaka 2018, takwimu zilizowahi kutolewa na gazeti la Mtanzania (unaweza ku-google ili kuthibitisha) zilionesha kwamba tangu mwaka 2016 hadi 2018 idadi ya madiwani wa Chadema waliojiunga CCM ilifikia 129 huku waliotoka CUF ikifikia tisa. Hapo wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitingoji hawakutajwa.

Kwa harakaharaka, baadhi ya wanasiasa waliopita Chadema na ambao sasa hawapo nilikuwa ninajaribu kuwakumbuka nikapata wengi sana ninahisi kuna wengi nimewasahau. Miongoni mwa viongozi makini waliokwishaihama Chadema ni Profesa Kitilia Mkumbo, Samsoni Mwigamba, David Kafulila, Patrobas Katambi, Albert Musando, Edna Sanga na Zitto Kabwe.

Pia wamo Peter Lijualikali, Joshua Nassari, Moses Machali, Dk. Godwin Mollel, Mwita Waitara na Julius Kalanga. Lakini Chadema pia imekimbiwa na watu kama Pauline Gekul, James Millya, Joseph Mkundi, Marwa Chacha na wengine ambao siwakumbuki.

Kwa nini wanahama? Unaweza kuwasikia waliobaki Chadema wakisema wanaohama ni kwa ajili ya tamaa na njaa. Hayo ni maneno ya kujifariji tu lakini ukweli unabaki kwamba wanahama kwa sababu ya muundo na ujendeshaji mbovu wa chama hicho.

Ndani ya Chadema ukiangalia kwa umakini, mundo wake hautoi fursa kwa watu wapya kupenya nafasi za juu tofauti na Chama Cha Mapinduzi. Lakini baya zaidi ni chama kimegeuka kama genge la watu wachache kama si Saccos ya mtu na kuendesha chama kuridhisha mapenzi ya huyo mtu na washikaji wake badala ya kuacha demokrasia ifanye kazi.

Mchungaji Msigwa anasema: "Ndani ya takribani miaka 20 nimejitahidi kuzungumza haki, demokrasia na Uhuru ndani ya Chadema lakini sijaviona kwani mambo hayo imekuwa ni propaganda tu, hakuna ukweli kwamba yanafanyika ndani ya chama, na mimi napenda ukweli," anasema.

Msigwa anasema baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, amekuja na falsafa ya 4R zinazohusu kustahimiliana, kufanya maridhiano, kufanya mabadiliko yenye tija na kujenga nchi upya na kwamba mtu yeyote muungwana na mwenye mapenzi na nchi lazima aunge mkono falsafa hiyo.

"Mimi nimejiunga na CCM baada ya kuona mambo tuliyopigania kwa mda mrefu yanayafanywa kwa weledi ndani ya CCM, mfano, mikutano ya hadhara (yenye kuzungumza hoja zanye faida kwa wananchi), uhuru wa mawazo, uhuru wa vyombo habari na katiba yenye kufuata sheria lakini Chadema vyote hivyo havifuatwi nami roho yangu imenisuta kuikemea Serikali ya CCM wakati sisi Chadema hatutendi haki," anasema Msigwa.

Ni katika muktadha huo, Msigwa anawataka Watanzania, hususani vijana kusoma alama za nyakati kwamba Chadema imepoteza dira na haieleweki inataka nini.

"Ndugu zangu tuchague CCM ndicho chama kinachojishughulisha na shida za watu. Mie nimeona mfano hata kule Iringa mambo makubwa yamefanyika," anasema Mchungaji Msigwa.

Kimsingi anayosema Msigwa yalishasemwa zaidi ya miaka 10 iliyopita kupitia Waraka wa Mkakati wa Mabadiliko uliosababisha akina Zitto Kabwe wakafukuzwa Chadema.

Walisema waziwazi kwamba sasa hivi chama hicho ni Saccos ya mtu, kuna ubadhirifu wa kutisha na hakuna demokrasia wala mbinu mpya za kukifanya chama kuungwa mkono zaidi ya kufanya maandamano yasiyo na tija.

# Chadema karibuni kilingeni, ila mjipange!

**Na Hamid Yassin**

NIMEMSIKIA Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe akinena kwamba, safari hii kamwe hawatasusia uchaguzi wowote ule na kusisitiza watashiriki kikamilifu chaguzi zote.

Naamini hapa Mbowe anaamanisha huu uchaguzi ujao baadaye mwaka huu wa Serikali za Mitaa, kwani Chadema tangu iasisiwe haijawahi kususia ule Uchaguzi Mkuu wa nchi!

Ukiondoa zile chaguzi mbili za kwanza za mwaka 1995 na ule wa 2000 ambazo Chadema hakikusimamisha wagombea urais lakini si kwa kususia bali kwa kujipanga; hiyo ni kwa mujibu wa kauli ya mwasisi wa chama hicho, Mzee Edwin Mtei kwamba, walikuwa wanakijenga chama kwanza.

Kuanzia hapo chama hiki hakijawahi kuacha kusimamisha mgombea uraisi katika chaguzi zote zilizofuata, zaidi ya kususia mara kadhaa zile chaguzi ndogo za udiwani, ubunge na Serikali za Mitaa kama walivyofanya mwaka 2019.

**MGOMBEA URAIS WA KWANZA**

Kuanzia mwaka 2005 Chadema ilianza kusimamisha mgombe urais na ambaye alikuwa wa kwanza ni huyu Mwenyekiti wao wa sasa, Mbowe ambaye alishika nafasi ya tatu kwa kuambulia asilimia 5.88 ya kura zote zilizopigwa mwaka huo.

Mwaka 2010 Mbowe akaona maji marefu, akaamua kumkabidhi kijiti cha kuwania urais aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Wilbrod Peter Slaa ambaye angalau alijikongoja kwa kupata kura 4,627,923 sawa na asilimia 27.1 ya kura zote halali zilizopigwa.

Ndiyo maana nasema Mbowe anaposema kuanzia sasa hawatasusia chaguzi, bila shaka anamaanisha huu wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba mwaka huu.

**KARIBUNI KILINGENI!**

Hii maana yake Chadema kinaacha tabia ya kuwaminyia wanachama wake wa ngazi za chini kushiriki katika chaguzi za nchi kama ambavyo naamini Katiba yao inataka sambamba na ile ya nchi.

Wanachama wao wa ngazi ya chini? Ndiyo! Mara nyingi Chadema huwa inasusia zile chaguzi ndogo za marudio zinazohusisha madiwani, wabunge na kama huu wa Serikali za Mitaa, lakini linapokuja suala la kushiriki Uchaguzi Mkuu wa nchi hapa huwa hakuna muamana, lazima washiriki!

Kwa nini? Jibu ni rahisi tu, kwa sababu wakubwa wa chama hiki ndiyo hupata nafasi ya kugombea na wakibahatisha wabunge wanakuwa na uhakika na ruzuku ya serikali!

Hivi unajua pamoja na kuwakataa wale wabunge wa viti maalumu lakini ruzuku iliyotolewa kwa ajili yao wametia kibindoni kimyaaa!!

Kwenye Uchaguzi Mkuu huwezi kusikia masuala ya kudai Katiba mpya wala Tume Huru ya Uchaguzi, lazima watie timu uwanjani!

**ZINGATIENI NASAHA HIZI**

Ninachowasihi Chadema ni kuingia kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa amani na utulivu, na si kuanza kutengeneza mazingira ya fujo wakati wa kampeni, siku ya uchaguzi, siku ya kutangaza matokeo na hata baada ya zoezi zima la uchaguzi kumalizika.

Kwa nini nasema hivi? Kwenye mkutano huo huo wa Chadema ambao Mbowe alitangaza kwamba kuanzia sasa watashiriki chaguzi zote, Mwenyekiti wa chama hicho Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema aliibuka na kauli za kichochezi!

Kiongozi huyu mwandamizi wa Chadema aliunga mkono kauli ya Mwenyekiti wake ya kushiriki kwenye uchaguzi huo, lakini akaibuka na kauli za kwamba mtu



Tundu Lissu na Freeman Mbowe wakiwa kwenye mkutano.



Moja ya maandamano ya Chadema.

yeyote atakayewaibia kura watamshughulikia!

"Tutashiriki chaguzi zote na tuna uhakika wa kushinda, atakayethubutu kutuibia kura zetu sisi Chadema tutamuiba yeye," aliongea Lema huku akishangiliwa na wafuasi wa chama hicho!

Ni vema kusikia Chadema wakisema watashiriki chaguzi zote zijazo, lakini changamoto kubwa zinazotokea mara kwa mara na kusababisha upotevu wa amani ni viongozi hao kushindwa kutimiza wajibu wao kwa kutoa kauli za uchochezi kama hizi za Lema.

Kimsingi chaguzi za Tanzania huwa zinaendeshwa kwa amani na kufuata kanuni zote ambapo vyama vyote huwa na mawakala kwenye vituo. Na siku chache kabla ya chaguzi vyama hukutana na kupeana miongozo inayoonesha mambo ya kufuatwa.

**KUJAZA WAFUASI UPEPO**

Desturi ya kuwajaza 'upepo' wafuasi wao halafu baadaye kushindwa kuwadhibiti, ama kwa kuogopa kuonekana wasaliti, au kwa akili ndogo zisizoweza kupima athari za mihemuko hasi au kwa dhamira mahususi ya kuwatoa kafara kwa ajili ya manufaa ya kisiasa ya chama au viongozi wake, matokeo yake huwa lawama kwa Serikali na vyombo vyake vya dola!

Kwa bahati sana siku zote viongozi wakuu wa vyama vya upinzani wamekuwa wachochezi wakubwa wa vurugu za wafuasi wao kutokana na kauli zao za kisiasa zisizojali maslahi ya umma kama hiyo ya Lema. Na mara nyingi zaidi viongozi wanaohusika zaidi ni wale wakuu.

Wakati siku zote viongozi wa kati wamekuwa wasimamizi wazuri wa hisia za wafuasi wao, wale wa juu zaidi wamekuwa wavurugaji wakubwa huku wakijua wazi kwamba mwisho wa vurugu zozote watakazozisababisha watakaoathirika zaidi ni wafuasi wao na jamii kwa ujumla.

Ili kueleweka kirahisi nitatoa mifano kadhaa ya yaliyowahi kutokea katika chaguzi za huko nyuma kuanzia zile za mwaka 2000.

Machafuko makubwa yalitokea Zanzibar na kusababisha vifo, vilema, na mamia ya watu kukimbilia ughaibuni kama wakimbizi. Yalikuwa ni machafuko ya kisiasa tu ambayo bila shaka yalichochewa na viongozi wa kisiasa.

Kimsingi viongozi wakuu wa Chama cha Wananchi (CUF) wakati ule hawakuwa waathirika wa kadhia ile kama ilivyowakuta wafuasi wao. Kwao tukio lile liliwaongezea tu umaarufu ndani na nje ya nchi.

**MAALIM SEIF AWEKA MSIMAMO**

Baada ya uchaguzi wa 2010 mambo kama yale ya vurugu na uchochezi yalitaka kujirudia tena. Wafuasi wa CUF wakiamini kwamba aliyekuwa mgombea wao, marehemu Maalim Seif Sharif Hamad alishinda lakini akadhulumiwa walifanya mashinikizo mengi kwa viongozi wao wakitaka waruhusiwe kufanya maandamano makubwa na vurugu huko Zanzibar.

Kwa kauli yake, marehemu Maalim Seif mbele ya waandishi wa habari katika ukumbi wa Shaaban Mloo, Buguruni jijini Dar es Salaam akasema kamwe asingeweza kuruhusu maandamano hayo kwa vile bado alikuwa na kumbukumbu ya yaliyotokea 2001.

Akasema kama mzazi hawezi kwa vyovyote kumruhusu mtoto wake abebe jiwe kwenda kupambana na askari mwenye bunduki na mabomu. Alijua kwamba kwa vyovyote mwishowe atakayeathirika ni mtoto wake jambo ambalo halingemfaidisha chochote zaidi ya umaarufu wa kisiasa.

Kwa kukataa kule kuruhusu maandamano marehemu Maalim Seif alifikia kutiliwa shaka kwamba ni msaliti. Eti alikuwa anatumika kwa maslahi ya CCM. Lakini yeye akasema bora shaka hizo kuliko kuwatoa vijana wake kafara katika ukomavu wake wa kisiasa.

**MACHAFUKO ARUSHA**

Miaka kadhaa baadaye chama Chadema kikafanya mambo ya ajabu kidogo kule Arusha. Mbele ya viongozi wake wote wakuu wa kitaifa, wafuasi wao wakashinikiza kwenda kituo kikuu cha polisi mkoani humo kwenda 'kuwakomboa: wenzao waliokuwa wakishikiliwa.

Katika hali ya kushangaza zaidi viongozi nao chini ya mwenyekiti wao Mbowe wakaridhia na kuungana na wafuasi wao katika maandamano hayo. Pengine waliamini wangeweza kupambana na Jeshi la Polisi, kuteka kituo na hatimaye kuwatoa watu wao.

Bila shaka sote tunayakumbuka yaliyofuatia. Sina hakika na kiwango cha umaarufu walichokipata kutokana na vurugu zile lakini kichapo walikipata. Wengine walipoteza maisha, wengine walipata vilema vya kudumu na wengine walipata athari za namna nyingine.

Wapo mabinti wawili waliokuwa wakitika madrasa walikumbwa na vurugu na mmoja alikatwa mguu. Kuna siku inshaAllah tutaleta kisa chake humu.

Hawa walikuwa viongozi wakuu wa chama ambao walikosa busara ya kudhibiti hisia za wafuasi wao kama kweli hawakuwa wao waliozichochea.

Hata hivyo, yapo matukio mengine ambayo yanathibitisha hekima walizonazo baadhi ya viongozi katika vyama hivyohivyo japokuwa wanazidiwa nguvu na wale wasio na hekima.

Na kwa bahati mbaya katika vyama hivyo kutumia hekima na kuepusha mihemuko ya ovyo ya wafuasi inaweza kuonekana ni usaliti. Na hii ndiyo athari ya kuchukulia ushindani wa kisiasa kama harakati za ukombozi za taifa lisilo huru.

**SI RAHISI ABADANI**

Tukiacha haya mambo ya vurugu, kingine muhimu ambacho Chadema wanapaswa kukijua na naamini wanajua, ni kwamba, kushinda uchaguzi dhidi ya CCM ni kazi pevu sana.

CCM kutokana na ukomavu wake si rahisi kupoteza uchaguzi kwa matokeo ya jumla; wapinzani wanaweza wakapa viti kadhaa vya ubunge kwenye chaguzi, wakashinda viti kadhaa kwenye viti vya udiwani, kadhalika na kwenye Serikali za Mitaa, lakini si kushinda uchaguzi!

Hii inatokana na jinsi chama hicho tawala kinavyojitahidi kutekeleza sera zake na kupanga karata zake huku vyama vya upinzani vikiendelea kukosa mvuto kwa kushindwa kuonesha sera mbadala na pia kukosa demokrasia ndani ya vyama hivyo.

Kwa kukosa mvuto, demokrasia ya ndani huku kikihubiri mambo ambayo chenyewe hakina, Chadema inaendelea kukimbiwa na viongozi wake makini na kubakiwa na magalasa!

Kama na wewe ni muumini wa uchambuzi wa kiasi 'quantitative analysis', utakubaliana na hiki ninachokisema. Hebu tuangalie data zinatuambia nini kwa uchaguzi ule wa kwanza na zilizofuata tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi hapa Tanzania 1992.

Baada ya kuanzishwa mfumo wa vyama vingi nchini taifa kwa mara ya kwanza lilikwenda kwenye uchaguzi 1995 uchaguzi ambao ulishirikisha vyama vingi vya siasa. Upinzani ulionekana mkubwa kwa watu wawili Hayati Benjamini William Mkapa na marehemu Augustine Lyatonga Mrema japokuwa vyama vingine pia vilikuwepo.

Katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 29, 1995 Mgombea wa CCM hayati Mkapa alipata kura 4,026,422 wakati mgombea wa NCCR-Mageuzi, Mrema alipata kura 1,808,616. Wapiga kura walikuwa ni 6,846,681. Hivyo, Mkapa alipata asilimia 61.82 wakati Mrema akipata asilimia 27.77.

Baada ya uchaguzi huo Mkapa aliingia madarakani na kuitoa Tanzania kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kwa kifupi ni kwamba Mkapa alifanya mambo makubwa sana katika kipindi chake cha kwanza jambo lililowapa wananchi imani kubwa sana juu yake na kumrudisha kipindi cha pili kwa ushindi mkubwa zaidi ukilinganishwa na ule wa mwaka 1995.

Hakuna haja ya kuorodhesha mambo aliyoyafanya Mkapa hapa kwani kila mtu anayajua. Uchaguzi wa Mwaka 2000 CCM ilifanya vizuri zaidi kuliko miaka mitano nyuma.

Mkapa alipata asilimia 71.74 ya kura zote za Urais 5,863,201 wakati Prof. Ibrahim Lipumba wa CUF akipata asilimia 16.26 ya kura za Urais 1,329,077 wakati Mrema akigombea mara ya pili akipata kura 637,077. Wapiga kura waliojiandikisha wakiwa 10,088,484 na waliopiga kura wakiwa 8,517,598 sawa na asilimia 84.4.

Katika chaguzi zote hizi mbili Chadema hakikuwahi hata kushika namba tatu kwa sababu hakusimamisha wagombea.

Kutoka Uchaguzi ule wa kwanza wa vyama vingi hadi huu wa mwisho kufanyika mwaka 2020, rekodi za CCM kwenye kushinda chaguzi zimekuwa zikizidi kupanda huku kwa Chadema na vyama vingine vya upinzani zikisuasua ama kuporomoka kwa kiwango kikubwa.

Hivyo Chadema wanakaribishwa kilingeni kwenye hizo chaguzi zinazokuja, ila wajipange; la sivyo, watakuja kukutana na kimbunga kama si mafuriko yasiyozuilika kwa mikono!

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Ni mdahalo ama shambulizi dhidi ya Trump limemng'oa Biden?

**Na Mwandishi Maalumu**

KAMA ilivyotazamiwa kutokana na presha kuwa kubwa, hatimaye Rais wa Marekani, Joe Biden alitangaza kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha urais wa nchi hiyo ambao unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba.

Akitangaza uamuzi huo, Biden alisema imekuwa heshima kubwa zaidi ya maisha yake kuhudumu kama Rais wa nchi hiyo lakini ameamua kujiondoa huku akiamini kuwa ni kwa maslahi bora ya chama chake na nchi kusimama huku akiangazia kutimiza majukumu kama Rais kwa kipindi kilichosalia cha muhula wake.

Biden alilazimika kuweka barua kwenye mitandao ya kijamii baada ya wiki kadhaa za shinikizo kutoka kwa wanachama na wafuasi wa chama chake cha Demokrati, wengi wakitia shaka uwezo wake wa akili katika umri alionao wa miaka 81.

Uamuzi wa Biden kujitoa kwenye mbio za urais umekuja ikiwa imesalia miezi minne pekee kabla ya Wamarekani kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu.

Tatizo la uwezo wa Biden kuendelea kuongoza Taifa hilo kubwa na watu kuanza kumshinikiza ajitoe kwenye kinyang'anyiro hicho, hususani wanachama wenzake wa chama cha Democrati lilikuja baada ya kufanya vibaya kwenye mdahalo na mgombea wa chama cha Republican, Donald Trump mwezi uliopita.

Katika mdahalo huo, Biden alioneka kupata shida kujibu hata baadhi ya maswali rahisi na wakati mwingine matamshi yake yakiwa hayaleweki.

Hata hivyo, alijitetea kwamba aliingia kwenye mdahalo akiwa na uchovu kutokana na safari ndefu aliyoifanya mapema siku hiyo. Akawa anawaambia wanaomtaka aachie ngazi kwamba hawamtendei haki kumpima kwa mdahalo wa dakika chache na kusahau makubwa ambayo ameyafanya katika kipindi cha urais wake na anayoendelea kuyafanya huku akisema atamshinda Trump kwa sababu ni mgombea muongo.

Katika barua aliyoituma kupitia mitandao yake ya kijamii baada ya kuamua kubwaga manyanga, Biden amesema imekuwa ni fahari ya maisha yake kuhudumu kama rais.

"Japo ilikuwa ni azma yangu kuwania mhula wa pili, naamini itakuwa ni manufaa kwa chama changu na nchi mimi kujiengua na kujielekeza katika kukamilisha majukumu ya urais kwa kipindi kilichosalia cha muhula wangu."

Rais Biden pia amemshukuru Makamu wake, Kamala Harris, akisema alikuwa "mshirika wa kipekee."

"Na acha nitoe shukrani zangu za dhati kwa watu wa Marekani kwa imani na uaminifu mlioweka kwangu," taarifa yake iliongeza.

"Ninaamini leo na daima kwamba hakuna kitu ambacho Marekani haiwezi kufanya, tunapofanya pamoja, inabidi tukumbuke sisi ni Marekani."

Kama ilivyokwishadikezwa hapo awali, matokeo mabaya ya Rais Biden kwenye jukwaa la mjadala yalichochea sana ukosoaji mkubwa kuhusu uwezo wake wa kushinda uchaguzi.

Wasiwasi ulipozidi kuhusu uwezo wa kumshinda Trump na kuleta mvutano ndani ya chama cha Demokrati, jina la Kamala Harris likaanza kuibuka miongoni mwa orodha ya wagombeaji mbadala.

Kwa tangazo la Biden kwamba atahitimisha kampeni yake na kumuunga mkono, Bi Harris hatimaye sasa ni dhahiri mwanamke huyo amefikia nafasi ambayo alikuwa akitafuta kwa muda mrefu: kilele cha tiketi ya chama cha Demokrati na uwezekano wa kuwa rais.

Lakini safari ya Kamala Harris imekuwa ngumu na iliyojaa maswali magumu, haswa katika miezi ya hivi karibuni. Kwani pamoja na shinikizo dhidi ya bosi wake, Bi Harris alikuwa amechagua uaminifu mkubwa kwa Biden.

### URAIS KWA DAKIKA 85

Iwapo Kamala Harris atashinda uteuzi wa chama cha Demokrati na kuwa rais na kisha kushinda uchaguzi mwezi Novemba, atakuwa mwanamke wa kwanza kushinda urais wa Marekani.

Lakini haitakuwa mara yake ya kwanza kushika madaraka ya urais.

Huko nyuma mnamo mwaka 2021, wakati Joe Biden alipolazwa kwa upasuaji na kuchomwa sindano ya nusu kaputi ili afanyiwe uchunguzi wa kawaida wa utumbo mpana, Harris alishikilia madaraka kwa dakika 85.

Katika muda wake wa zaidi ya saa moja madarakani, Harris alitekeleza majukumu yake kutoka katika ofisi ya jengo la Magharibi mwa Ikulu ya White House.

### TRUMP NA UMRI MKUBWA

Mengi yamesemwa kuhusu umri wa wazee. Joe Biden na Donald Trump na jinsi wapigakura wanavyowaangalia.

Mtazamo huo ulikuwa zaidi kwa Biden mwenye umri wa miaka 81 ambaye mashaka na makosa yake yalikuwa gumzo hasa katika wiki baada ya mdahalo wa urais na Trump.

Donald Trump, mwenye umri wa miaka 78, sasa atamiliki taji lisilotakikana la 'mteule mzee zaidi katika historia ya urais' na atarithi suala la umri kutoka kwa Biden ambaye amejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kuingia Ikulu ya White House.

### MAMBO MATANO YANAYO

Kuna mambo matano ambayo yamekuwa yakifanyika tangu Biden ajiweke pembeni kuwania urais wa Marekani.

Mosi, Makamu wa Rais Kamala Harris aliungwa mkono na Joe Biden kuwa mgombea wa urais takriban nusu saa baada ya kutoa tangazo hilo na tayari ameanza kutuma barua pepe za kuchangisha pesa.

Pili, ActBlue, taasisi ambayo hutoa michango ya umma kwa wagombeaji wa Demokrati, inasema wafuasi wa ngazi ya chini sasa wamechangisha dola milioni 46.7 tangu uzinduzi wa kampeni ya Harris siku kubwa zaidi ya uchangishaji wa mzunguko wa 2024!

Tatu, Wanademokrati wenye jina kubwa wanamuunga mkono Kamala Harris kama mgombea wa urais anayepaswa kupitishwa rasmi na chama chao. Hawa ni pamoja na Gavana wa California Gavin Newsom ambaye aliwahu kupendekezwa kuwa mbadala wa Biden katika kipindi cha wiki chache zilizopita.

Nne, kujiondoa kwa Biden kunamaanisha kuwa mgombea mteule wa chama cha Republican, Trump sasa ndiye mteule mzee zaidi katika historia ya urais akiwa na umri wa miaka 78.

Tano, baadhi ya wafuasi sugu wa Trump, akiwemo Marjorie Taylor Greene na Greg Abbott, wamesema mtu wao anaweza kumshinda kirahisi Harris kwenye uchaguzi wa Novemba.

### TRUMP ANAWEZA KUMSHINDA HARRIS?

Wakati Demokrati wakipa mbana kutafuta mteule mpya, Trump pia anapambana kutafakari kuhusu ripoti ya hivi karibuni kutoka jarida la 'The Atlantiki' inaonyesha kiwango ambacho kampeni ya Trump ilikuwa kukabiliana na Joe Biden katika uchaguzi.

Kwa hivyo sasa atajiuliza kampeni za Republican zitafanya nini dhidi ya Makamu wa Rais Kamala Harris, ikiwa yeye ndiye atapitishwa rasmi kuwa mgombea mpya wa Demokrati?

Mtu mmoja kutoka kampeni ya Trump alitumia ujumbe wa maandishi akisema wanahisi rais huyo wa zamani anaweza kumshinda Harris. Mtu huyo anaona, kama si mdahalo na baadaye jaribio la kumuua Trump lililomwingezea umaarufu, Biden alikuwa mgombea mgumu kumshinda kuliko Bi Harris.

*Inaendelea uk. 18*



Kamala Harris

# Fanyieni kazi ushauri huu kupata wagombea bora



Ridhiwani Kikwete

**Na Dk. Reubeni Lumbagala**

Kwa mujibu wa falsafa ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ili nchi iweze kupata maendeleo ya kweli inahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Kwamba uwepo wa mambo haya manne na yakatumika kikamilifu kunaweka uhakika wa jamii na nchi kwa ujumla kupata maendeleo ambayo ndiyo kiu kubwa ya kila mwananchi.

Wananchi wanataka maendeleo na ustawi bora ili kufurahia zawadi ya maisha hapa duniani. Ndiyo maana wananchi wanajituma kila siku katika shughuli za uzalishajimali ili kupata vipato vitakavyowawezesha kukidhi mahitaji yao na kupiga hatua za kimandeleo.

Tukirudi katika mambo manne aliyoyasema Hayati Baba wa Taifa ili nchi iweze kupata maendeleo, kwa leo nataka nizungumzie eneo moja la uongozi bora kama chachu ya kufikia maendeleo. Uongozi bora ni kuongoza kwa kufuata kanuni na sheria kwa manufaa ya wale wanaoongozwa.

Uongozi bora ni ule wenye kuzingatia mahitaji ya watu, kujituma, kupigania haki kwa kuhakisha maslahi ya wengi yanazingatiwa. Aidha ni uongozi unaosikiliza hoja za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. Uongozi bora hauna ubinafsi wala umimi, bali unasimama na mahitaji ya wananchi.

Maendeleo ya kweli katika jamii na nchi kwa ujumla yatapatikana endapo wananchi watachagua viongozi bora ambao watasimama na kupigania haki na mahitaji ya wananchi na si mahitaji binafsi ya kupata umaarufu na kujilimbikizia mali.

Mwishoni mwa mwaka huu, nchi yetu inatarajia kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa na mwakani uchaguzi mkuu. Uchaguzi ni njia ya kidemokrasia ya wananchi kuchagua viongozi bora watakaowatumika na kuwa daraja la kufikia maendeleo.

Uchaguzi ni fursa kwa wananchi kusema nani wana imani naye na kuamini kuwa anaweza kukidhi matarajio yao na kujenga jamii na nchi yenye amani na maendeleo.

Ndiyo maana ni muhimu kwa wananchi kushiriki kikamilifu kwa kusikiliza sera za wagombea ili kufanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi ndani ya mchakato wa ndani wa vyama vya siasa na mwisho katika uchaguzi wa jumla unaohusisha wagombea kutoka vyama vyingine katika eneo husika.

Kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wananchi kuwalalamikia viongozi wao, lakini cha ajabu baadhi ya wananchi hao wanaolalamika ndiyo hao hao ambao hawakushiriki kupiga kura na hivyo wanaongozwa na viongozi waliochaguliwa na watu wengine!

> **Lakini kutafuta wale marafiki zenu ambao mnauza nao mapori, kutafuta marafiki zenu mnaofanya nao ubadhirifu wa mali za umma, ni kukiingiza chama kwenye mtihani mkubwa sana.**

Hivyo basi, njia nzuri ya kupata viongozi bora ni wananchi wenyewe kushiriki kuwasikiliza wagombea na mwisho kufanya maamuzi sahihi ya kuchangua viongozi kwa vigezo madhubuti vya kupata viongozi bora na si kwa mazoea au kuhongwa na wagombea.

Mwanamajumui wa Kenya, Profesa Patrick Loch Lumumba alipata kusema kwamba wakati wa uchaguzi ni sawa na mtu kupewa hundi (blank cheque) ili aandike mwenyewe anachotaka.

Kwa hiyo vyama vinapopitisha mgombea mbovu na hatimaye wananchi kumchagua wanakuwa wametumia vibaya hundi hiyo muhimu.

Profesa pia huwa anawashangaa Waafrika kuchagua viongozi wabovu na kisha kulalamika akisema ni sawa na kununua pikipiki na kutarajia ifanye kazi kama benzi!

Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ni chama tawala kina kiu ya kutaka kuendelea kuwatumikia wananchi katika kipindi kingine cha miaka mitano katika chaguzi zote yaani uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu na ule mkuu wa mwakani.

Kumekuwa na ushauri mbalimbali unaotolewa na viongozi wa chama kuanzia ngazi za juu, kati hadi chini kabisa ya namna bora ya kufanya ili kushinda chaguzi hizi.

Wanachama wa CCM nao katika nyakati tofauti tofauti nao wamekuwa na maoni na ushauri kadha wa kadha ili kukisaidia chama kuibuka kidedea.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Chalinze Ridhiwani Kikwete hakubaki nyuma katika kushauri njia bora ya kufanya ili kukiwezesha chama chake kuibuka kidedea bila kutumia nguvu kubwa na kupata ushindi mapema kabisa.

Hivi karibuni, akiwa kwenye mkutano wa wananchi wa Mkange wakati wa ziara yake jimboni kwake aliwaasa wananchi kuacha kuchagua viongozi kwa kujuana au kwa nguvu ya fedha.

Ridhiwani Kikwete alitoa nasaha hizi alipokuwa akihamasisha wananchi kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ambao ni msingi wa kupata viongozi bora watakaokuwa chachu ya maendeleo katika maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

"Hata kama kuna mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi ambaye yeye mwenyewe mnamwona wala hataki mambo hayo, jamii pale inamtaja vizuri, mfuateni na mumwambie kama wewe mwenzetu kila tukikaa kijiweni tunasema kama kuna mtu mzuri wa kutuongoza basi ni yule pale ambaye ni wewe utatuletea mambo mazuri eneo letu.

"Basi mfuateni na mwambie ili kukisaidia chama chetu. Lakini kutafuta wale marafiki zenu ambao mnauza nao mapori, kutafuta marafiki zenu mnaofanya nao ubadhirifu wa mali za umma, ni kukiingiza chama kwenye mtihani mkubwa sana," amesema Ridhiwani Kikwete.

Alichosema Ridhiwani Kikwete ni jambo la msingi sana na linapaswa kuzingatiwa na viongozi na wanachama wa CCM kwani mara nyingine wananchi na wanachama wa CCM wamekuwa wakipiga kura za hasira kwa vile tu hakusimamishwa mgombea aliye chaguo la wananchi na hivyo kukidhoofisha chama chao.

Wanachama ndiyo wenye chama na si viongozi, hivyo basi wanachama wahakikishe wanakuwa na jicho la tatu la kuangalia nani anafaa kugombea na kupeperusha bendera ya chama na pale inapobidi wamshawishi mwanachama ambaye anao uwezo wa kuongoza lakini ni kama hayupo tayari kugombea.

Mwanachama ambaye huombwa na wananchi baada ya kuona uwezo wake na uadilifu wake mara nyingi huwa mzuri kuliko yule anayejipendekeza mwenyewe kugombea, tena yule anayepita akigawa hiki na kile kwa wananchi (kuhonga) ni hatari zaidi kwani atakalia kutaka kurudisha gharama zake badala ya kuwatumikia wananchi. Mwalimu Nyerere aliwahi kukemea sana mgombea wa aina hii.

Ni vyema sisi wananchi ndio tumgharamikie huyo mgombea kama kuna gharama kama za kampeni hata kumshonea suti kwani anakwenda kutufanyia kazi sisi.

Hii yote ni kutengeneza mazingira ya uhakika wa ushindi pindi mgombea huyo atakapopambana na wagombea wa vyama vingine. Katika kusisitiza na kukazia hoja yake, Ridhiwani Kikwete anasema, "Ninaamini viongozi ninyi ambao ni wanachama hamtafanya kosa hilo. Tuleteeni watu ambao tukifika hapa watu wanaendelea na shughuli zao tukisubiri siku ya kupiga kura, tunapiga kura na maisha yanaendelea."

Naamini tumeelewa alichokisisitiza Ridhiwani Kikwete, cha muhimu ni wananchi kuchagua viongozi bora wanaokubalika katika jamii ambao watakuwa nyenzo ya kufikia maendeleo ya kweli, na hao ndiyo wanaotakiwa katika ujenzi wa Tanzania tuitakayo yenye amani, upendo na maendeleo.

Kwa kuzima maneno ya Mwalimu Nyerere, wanachama wa CCM tupendekeze mgombea kwa kila nafasi ambaye mtu akikuuliza unadhani huyu atakuwa kiongozi mzuri, huyu ni mwadilifu, huyu ni mtenda haki, huyu anajua matatizo yetu, jibu litoke moyoni kabisa kabisa na si kwenye ulimi kwamba NDIYO.

*Dk. Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: 0620 800 462.*



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Tanga changamkieni fursa adhimu kilimo cha viungo

Tangu tumepata uhuru hadi sasa kilimo kinatajwa kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania. Hii inatokana na ukweli kuwa wananchi wengi hapa nchini zaidi ya asilimia 65 wanajishughulisha na kilimo au wanapata maisha yao kutokana na kilimo.

Kilimo kina dhima ya kutupa chakula Watanzania, kutupa mali ghafi kwa ajili ya viwanda lakini pia kinachangia katika kutupa fedha za kigeni kwa kuuza mazao nje.

Kwa hiyo Watanzania wanalima mazao mbalimbali ya biashara kama pamba, chikichi, mpunga, korosho na mengineyo sambamba na matunda, viungo na mbogamboga.

Lakini pia wakulima wa Tanzania wanazalisha mazao ya chakula kama mpunga, mhogo, maharage na jamii nyingine za kunde, mtama, uwele na kadhalika.

Wananchi wengi hasa wa vijijini na wachache wa maeneo ya mijini wamejiajiri kwenye kilimo na hivyo wanamudu kupata chakula na fedha kwa njia hiyo baada ya kuuza mazao yao. Serikali hukusanya ushuru na kodi na pia, kama nilivyosema awali, kupata fedha za kigeni kupitia uuzaji wa mazao nje ya nchi.

Pamoja na kwamba idadi kubwa ya wananchi wanaojishughulisha na kilimo wapo maeneo ya vijijini, lakini fursa zinazotokana na kilimo zinaweza kufanyika hata maeneo ya mijini na kwenye majiji. Unaweza kuniuliza inawezekanaje kulima mjini au jijini kabisa ambako hakuna ardhi kubwa ya kulima? Fuatana nami uelimike.

Kimsingi, kilimo kinaweza kufanyika hata katika eneo dogo kuzunguka makazi ya mtu na mtu akaweza kupata fedha. Mathalani, mtu anaweza kupanda mbogamboga kama mchicha, matembele, mchunga au kabichi.

Watu wanapanda mbogamboga hadi kwenye maghorofa kwa kutumia mbinu za kisasa za chupa, magunia na makopo na kuzalisha kwa wingi pale wanapoamua kulima eneo dogo kitaalamu.

Lakini, licha ya udogo wa eneo watu pia wanaweza kupanda miti ya matunda kama mipapai, mipera, miembe, michungwa na wakaweza kuvuna na wakapata fedha za kuendesha maisha yake kwa kuuza mazao.

Ukienda pale Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa mfano, sasa hivi wanatoa miche ya kisasa inayotia matunda ndani ya muda mfupi sana.

Mtazamo kuwa kilimo ni lazima kifanyike kijijini katika eneo kubwa umepitwa na wakati, muhimu ni kulima kisasa kwa kutumia mbinu za kisasa za kilimo kama vile mbegu bora, kutumia samadi na kumwagilia maji ya kutosha ya kuwezesha ukuaji wa mazao hayo, hivyo hata eneo dogo tu la kuzunguka nyumba yako unaweza kupiga hela mtu wangu hapo hapo ulipo Jijini Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza au hata Mbeya.

Baadhi ya wakazi wajanja wa maeneo ya mijini hasa kwenye manispaa na majiji wameanza kujishughulisha na kilimo kidogo (small scale griculture) ndani ya makazi yao au nje kidogo ya miji yao kutokana na uwepo wa fursa ya kujiingizia fedha kupitia kilimo.

Na hapa kipekee kabisa nimpongeze Mbunge wa Tanga Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Waziri wa Afya, Ummy Ally Mwalimu kwa juhudi zake za kuwainua kiuchumi wananchi wa Jiji la Tanga katika fursa za kibiashara akishirikiana kwa karibu na uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa kuweka mazingira wezeshi ya kuwainua wananchi.

Na pia Ummy Mwalimu amegeukia fursa ya kilimo katika kuwainua wananchi kiuchumi kupitia kilimo cha kisasa cha zao la viungo (spices). Mkoa wa Tanga umebarikiwa kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba ya kutosha inayostawisha mazao mengi kama vile mkonge, mahindi, mihogo, viazi, maharage, matunda na viungo, hali inayosaidia ongezeko la mapato katika mkoa wa Tanga.

Watu wa Tanga waliwahi kuwa na msemo wao kwamba kama mguu wa mtu ungekuwa unapandwa, basi kwa Tanga ungeota na kustawi!

Hivyo basi, wakazi wa Jiji la Tanga kwa upande wao licha ya kuwa mjini wanayo fursa ya kujishughulisha na kilimo kama njia ya kuboresha maisha yao na kuchangia maendeleo ya mkoa wao.

Kutokana na fursa zilizoko kwenye kilimo, Ummy Mwalimu ameipa kipaumbele sekta ya kilimo kwa wakazi wa Jiji la Tanga hasa kwa makundi ya vijana, wanawake na wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika kilimo cha zao la viungo na hatimaye kuboresha hali zao za kiuchumi.

Kutokana na umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika maendeleo, Halmashauri ya Jiji la Tanga imeamua kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Horticultural Association (TAHA) linalojishughulisha na kilimo cha bustani chenye kuzalisha mbogamboga, maua, viungo na matunda.

**Niwahakikishie Jiji la Tanga litashirikiana na ninyi (TAHA) kwa dhati kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Tutatumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya jiji kutoa mikopo kwa akina mama, vijana na walemavu waweze kulima kisasa na wanufaike.**

Shirika la TAHA linaweka mkazo wa kulima mazao kibiashara hata katika eneo dogo kwa kuzingatia kanuni bora za kisayansi ili kupata mazao mengi na bora kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje kwa ustawi wa wakulima na maendeleo ya nchi.

TAHA inatoa elimu bora ya kilimo kwa wakulima mbalimbali nchini ili kuwajengea uwezo na hatimaye kuwa wakulima bora ambao kilimo kitabadili hali zao za maisha badala ya kulima kilimo cha kujikimu pekee.

Julai 2, 2024, Halmashauri ya Jiji la Tanga chini ya uongozi wa Dk. Frederick Sagamiko ambaye ni Mkurugeniz Mtendaji wa Jiji la Tanga ilisaini hati ya makubaliano na TAHA ambapo Dk. Jacqueline Mkindi ambaye ni Mtendaji Mkuu alishiriki kusaini hati hiyo katika makao makuu ya taasisi hiyo jijini Arusha ambapo Naibu Meya wa Jiji la Tanga, Rehema Mhina alishiriki hafla hiyo pia.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Sagamiko alisema; "Lengo kuu la makubaliano yetu ni kubadilisha kilimo cha viungo kuwa cha kibiashara ili kutengeneza ajira za kinamama, vijana na wenye ulemavu katika jiji la Tanga."

Ikumbukwe kuwa ardhi ya Jiji la Tanga inastawisha vyema mazao mengi yanayotumika kama viungo na kwa muda mrefu kilimo hiki kimekuwa cha kawaida sana ambacho hakikuwa na mkazo katika suala zima la kulima kibiashara na ndiyo maana hali za maisha za wakulima wa viungo bado ni duni.

Baadhi ya mazao ya viungo ni kama iliki, mdalasini, pilipili mboga, pilipili manga, chai, vitunguu maji na vitunguu swaumu, tangawizi na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, ili kuongeza tija katika zao la viungo, kukuza ajira na kubadili hali za maisha ya wakulima wa viungo jijini Tanga, ushirikiano huu umekuwa muhimu sana katika kuhakikisha kilimo cha viungo kinakuwa cha kisasa kwa maendeleo endelevu.

Ili kufanikisha makubaliano haya kwa maendeleo ya zao la viungo, Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa kuanzia imetenga ekari tano kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kisasa kwa ajili ya kusindika na kuhifadhi viungo kabla ya kusafirishwa kwenda kwenye masoko ya nje.

Vilevile, Halmashauri ya Jiji la Tanga imetenga shamba la ekari 100 kwa ajili ya kilimo cha kisasa cha viungo. Kimsingi, wakazi wa Jiji la Tanga wanayo fursa ya kubadili maisha yao kupitia ushiriki wao kwenye kilimo hiki cha kisasa cha viungo. Huu ni uwekezaji mkubwa uliofanywa kwa manufaa yao kama juhudi za kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu. Mazao yanayotoa viungo mbalimbali kwa ajili ya mapishi yana soko kubwa ndani na nje ya Tanzania, hivyo suala la masoko si tatizo kabisa.

Ni muhimu kuzingatia kuwa suala la usindikaji na uhifadhi wa mazao ya viungo ni jambo la muhimu sana katika kuhakikisha yanabaki kuwa na ubora wenye kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa bila kuleta uharibifu.

Dk. Mkindi anaihakikishia Halmashauri ya Jiji la Tanga kufanikiwa katika uhifadhi wa mazao ya viungo kupitia Mradi wa Tuhifadhi Chakula unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID).

Kutokana na umuhimu wa elimu ya kilimo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa ubora, TAHA inawahakikishia wakulima wa Jiji la Tanga kupata elimu bora ya kilimo ili mazao ya viungo yaweze kuboresha maisha yao na kuongeza mapato na fedha za kigeni. Rehema Mhina ambaye ni Naibu Meya wa Jiji la Tanga anasema: "Niwahakikishie Jiji la Tanga litashirikiana na ninyi (TAHA) kwa dhati kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Tutatumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya jiji kutoa mikopo kwa akina mama, vijana na walemavu waweze kulima kisasa na wanufaike."

Ushirikiano wa viongozi na wananchi katika kufanikisha mipango ya maendeleo ni jambo jema, hivyo, wakulima wa viungo wa Jiji la Tanga washirikiane kikamilifu na viongozi wao katika kuhakikisha wanalima kisasa na kwa tija kwa maendeleo endelevu.

Kwa hakika, kilimo cha kisasa cha viungo kwa wakulima wa Jiji la Tanga kinakwenda kuleta tija ya ongezeko la ajira na mapato. Kilimo hiki kinakwenda kuufungua mkoa wa Tanga kibiashara na kuchochea ongezeko la fedha za kigeni kwa kuuza viungo nje ya nchi na kuchangia pato la Taifa.

Kwangu mimi, kilimo cha mazao ya viungo kwa wakulima wa Jiji la Tanga ni fursa adhimu ambayo haipaswi kuchezewa badala yake ichangamkiwe kutokana na kuwa na manufaa tele kitaifa na kimataifa.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# TABIA UNAZOTAKIWA KUZIACHA HARAKA ILI KUSONGA MBELE



**1. ACHA KUPENDA KUWARIDHISHA AU KUWAFURAHISHA WATU.**

Hili ni tatizo kubwa kwa jamii yetu hususan jamii za kijamaa ambazo watu wanaishi kama ndugu. Watu wanapenda maoni ya watu na wanajaribu kumfanya kila mmoja aridhike. Tabia hii itakufanya ujitahidi kufanya wanavyotaka watu na mwisho kujikuta uko kama wao.

Tabia hii inakuondolea upekee wako (Uniqueness) ambayo ni moja ya siri kubwa za kufanikiwa. Ukitaka kusonga mbele, hakikisha wazo lako, lipime kwa vipimo sahihi (smart) kisha jiamini na usonge mbele (Be yourself).

**2. ACHA KUJILINGANISHA NA WENGINE (NEVER COMPARE YOURSELVES WITH OTHERS).**

Kwenye maisha unahitaji kufanya tofauti ili kupata matokeo tofauti. Ukitaka kujilinganisha na wengine tegemea matokeo waliyoyapata.

**3. ACHA KUJISHTUKIA –**

Ukiamua kufanya jambo, anza hatua za kufanya, acha kujistukia na kujiona kama huwezi. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa wazo lako ni sahihi. Hakuna siku utajiona unaweza, unachotakiwa ni kuanza kisha katika safari unajenga uwezo. Wote wanaofanya makubwa, kuna siku waliamua na kuanza na ukiwauliza, watakwambia kuwa uwezo wao umeendelea kujengeka siku baada ya siku. Acha kujishtukia na kusitasita. Ukiamua anza na usonge mbele.

**4. ACHA KUKIMBIA CHANGAMOTO**

Vikwazo ni sehemu ya safari. Tafuta jinsi ya kutatua na si kukimbia. Hakuna kisicho na changamoto. Hata ukiamua kulala siku mbili utapata changamoto tu ya kuumwa mbavu. Usikimbie changamoto kabiliana nazo kwa kutafuta njia na kuzitatua.

**5. ACHA KUJIDANGANYA/ KUJIRIDHISHA**

Mara zote Tafuta uhalisia ili ukupe njia sahihi. Usichukulie mambo kirahisi. Hakiki njia zako bila kudharau wala kuchukukulia poa. Kwa lugha rahisi hapa nasisitiza uwe makini na ufanye mambo kwa tahadhari na kumaanisha hata kama unachofanya ni kidogo.

**6. ACHA KUFANYA KAWAIDA (ILI MRADI)**

Mara zote fanya kwa ubunifu, maarifa na ustadi. Tambua chochote kisichokuuma hakitawagusa wengine. Ukifanya mambo kiholela matokeo yake ni holela pia. Unapofanya jambo, tuliza akili, kuwa mbunifu, jiulize maswali mengi, wekeza nguvu ili upate kilicho bora.

**7. KUTOFANYA MAANDALIZI YA KINA**

Jiandae vizuri kwa kila kilicho mbele yako. Maandalizi mazuri yanakupa urahisi na manufaa makubwa kwenye kulifanya jambo. Mfano mchezo wa dakika 90 wa mpira, unaweza kuandaliwa mwezi mzima. Mchezo wa ngumi wa round nane, unaandaliwa miezi mitatu au zaidi. Hapa nakuonesha umuhimu wa kujiandaa na kitu unachokifanya.

**8. ACHA VISINGIZIO**

"Ukihitaji jambo utatafuta njia, lakini kama hutaki utatafuta visingizio". Hakuna kushindwa kunakokosa visingizio.

Ukitaka kufanikiwa, acha kutafuta visingizio (excuses). Kiri kushindwa na uangalie nini kilikufanya ushindwe kisha amua kuwa hutashindwa tena.

**9. ACHA UBINAFSI**

Njia yako inahitaji watu sahihi ambao una nafasi kwao nao wana nafasi kwako. Watu wanaweza kuwa sababu ya uimara wako au sababu ya anguko lako. Pamoja na angalizo hilo bado ukweli ni kwamba unahitaji watu ili kusonga mbele.

Unachotakiwa kufanya ni mambo mawili makubwa, acha ubinafsi na uchague watu sahihi.

**10. ACHA KULALAMIKA SANA**

Tabia hiyo inakufanya ujioneshe dhaifu usiye na uwezo wa kubadili hali ila unataka huruma za watu.

(You sound Powerless) Monitor your behavior.

**11. ACHA KUKOSOA KILA KITU**

Jifunze kuona mema zaidi kuliko mabaya (Positive Mindset). Huwezi kupata kitu usichokiona mara kwa mara. Ukiwa kila wakati unaona ubaya na kukosoa, hatuwezi kutegemea matokeo mema kwako. Badili mtazamo, kulalamika sana ni zao la mtazamo hasi.

**12. ACHA TABIA YA KUAHIRISHA MAMBO (PROCRASTINATION).**

Tabia hii inaweza kuwa moja kati ya tabia chache kubwa zinazowafanya wengi kutopiga hatua. Jiulize unapanga mambo mangapi na unatekeleza mangapi? Utagundua hata wewe ni mhanga na mwathirika wa ugonjwa huu mkubwa wa kuahirisha mambo.

**13. KUTAKA KUWA SAHIHI WAKATI WOTE (PERFECTIONISM)**

Ni muhimu sana kuhakikisha kuwa unakuwa sahihi, lakini kuacha kufanya mambo kwa ajili ya kutafuta usahihi tu kutakuchelewesha sana.

**14. ACHA TABIA YA KUSEMA "NDIYO" HATA MAHALI AMBAPO ULITAKIWA KUSEMA "HAPANA"**

Watu wengi tunadhani kusema ndiyo ni unyenyekevu au busara. Jambo la kwanza ni vizuri kila siku

uwe na ratiba ya mambo ya kufanya (To do list). Kama wewe una ratiba yako ya mambo ya kufanya, halafu kikija kitu kingine hutakubali kila kitu ili kutekeleza ratiba yako. Ndiyo yako iwe ndiyo kama una nafasi na kama huwezi au huna nafasi, sema hapana.

**15. ACHA MAWAZO (MTAZAMO) HASI YAANI KUONA KUSHINDWA TU**

- Negative Perception. Ni vizuri kuwa na muda kujiuliza wewe Unaona nini kwenye maisha. Huwezi kupata matokeo usiyoyaona kwenye mtazamo kwanza. Kama kuna vitu vya kuviacha kwa haraka ni mtazamo hasi.

**16. ACHA KUPUUZA MALENGO YAKO NA KUTOKA KWENYE NJIA**

(Lack of self Determination).

Siku zote timiza malengo usitoke kwenye lengo lako wala kuacha njia yako.

**17. ACHA KUWA NA MTAZAMO WA PESA KULIKO MATOKEO YA KULETA SULUHU YA TATIZO KWENYE JAMII.**

Wazo lako ni vizuri ukilipanga kwa kuangalia matokeo yake chanya kwenye kuwahudumia watu au kutatua tatizo fulani kwenye jamii. Wazo lolote linalolenga kutatua tatizo kwenye jamii litanunuliwa kwa gharama yoyote. Lakini mpango ukilenga fedha, inaweza kukusumbua.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi, Kikundi, Kanisa, Umoja, NGO au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

***We work Consult***
***Your Partner in Growth.***

# Malipo kielelekitroniki



Inatoka uk. 10

Hata hivyo, tukifanya kazi kwa bidi na kila mtanzania akawajibika ipasavyo; nchi yetu unao utajiri mwingi ikiwemo rasilimali ardhi na watu kuweza kijikwamua kimaendeleo.

Kiuhalisia taifa letu bado liko kwenye kuhangaikia maendeleo halisi na endelevu kwa wananchi wake. Kwa kiasi fulani tumepiga hatua lakini bado hali ni tete na hasa tukizingatia ukubwa wa taifa letu na ongezeko la watu pamoja na mifugo. Taifa fulani, linaweza likasifiwa kwa kuwaletea maendeleo watu wake lakini ukiangalia ukubwa wake na namba ya watu bado utaona kuna tofauti na taifa lenye eneo kubwa kama letu.

Mathalani, taifa lenye eneo dogo rasilimali zake pia ni haba ukilinganisha na lenye eneo kubwa kama Tanzania, rasilimali tele na kupakana na Bahari ya Hindi: zaidi ya kilomita 1,000 tukimiliki takribani rasilimali zilizomo ndani ya ukanda wa kilomita 200 baharini kutoka ardhi inapoishia ikiwepo rasilimali ya mikoko takribani hekta 150,000: zenye ikolojia ya kuzalia samaki na viumbe bahari wengine.

Kimsingi mapato ya Serikali yanatokana na wananchi na wawekezaji kwa kulipa kodi kama sheria husika inavyoelekeza. Kadhalika, uwezo wa kulipa kodi unatokana na kipato kinachotokana na matumiza ya ardhi kuzalisha mali kupitia, mfano, kilimo na ufugali, matumizi mbalimbali ya maliasili zilizopo, biashara, utalii, ujasiriamali, uwekezajia wa namna mbalimbali na huduma mfano, utalii.

Watanzania tunapoiweka Serikali madarakani tunatarajia itutumikie na kutuletea maendeleo tarajiwa. Kwa upande mwingine ni wajibu wetu kuhakikisha tunaiwezesha kwa kulipa kodi/tozo husika kufanikisha utekelezaji wa mipango husika kwa maendeleo tarajiwa.

Nadhani wengi tungependa kulipa kodi ili ndoto zetu kimaendeleo ziweze kutimizwa. Mathalani, tuneshuhudia wengi wakimiminika kutumia usafiri wa Reli ya kisasa ya mwendokasi (SGR) kwenda Morogoro ikiwa ni ishara njema ya matokeo ya juhudi za Serikali.

Kwa uzoefu tulionao changamoto za ulipaji kodi zimekuwa zikijitokeza sababu viwango vya kodi/tozo pamoja na jinsi ukusanyaji wake unavyofanyika; lakini siyo kuwa watu hawataki kulipa kodi/tozo husika.

Kadhalika, walipakodi wanapokuwa hawaoni nini kinafanyika kunajitokeza fikra za watu kujiuliza kwamba nalipa kodi ili iweje? Iwapo matumizi ya fedha za kodi/tozo yanapokuwa hayakizi viwango tarajiwa vya kimaendeleo; kunakuwepo na vinyogo kulipa kodi/tozo au inalipwa lakini haitekelezi kilichotarajiwa kutokana na ubadhilifu na/au kupotea fedha za umma kwa kukosa usimamizi thabiti.

Ni imani yangu kuwa iwapo kutakuwepo na usimamizi mzuri na uwajibikaji toshelezi pamoja na viwango vya kodi kuwa rafiki na njia za makusanyo pia zikawa rafiki, hakuna shaka Watanzania wengi watapenda kulipa kodi/tozo kwa maendeleo tarajiwa.

Huwa najiuliza msingi wa kuweka VAT asilimia 18 nini na siyo asilimia kumi au chini ya hapo? Bahati mbaya malipo haya yanahusu huduma na bidhaa nyingi sijui ni kitu gani hakitozwi VAT?

Watu wengi tunaoishi mijini maisha yetu yanategemea vyakula na vitu vya kununua kwenye maduka: kawaida na makubwa, pia kwenye masoko mathalani, Soko la Kisutu, Dar es Salaam au Kingalu, Morogoro. Natumaini wanaouza bidhaa madukani wanatakiwa watumie kifaa cha kielekitroniki (EFD). Serikali imekuwa ikisitiza: ukinunua dai risiti; ukiuza toa risiti hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwepo kukengeuka kuhusu matumizi ya kifaa hicho muhimu cha kuisaidia Serikali kupata mapato yake halisi.

Ukinunua bidhaa kwenye maduka makubwa Dar es Salaam mfano, Mlimani City, Masaki, Msasani, Victoria au Jijini-kati; mpokea fedha anapofungua sehemu ya kuweka fedha, hapohapo risiti inajitokeza kupitia kifaa kilichounganishwa na kompyuta ya mauzo.

Risiti inaonyesha mchanganuo wa kiasi kilicholipwa na VAT anayolipa mnunuzi kulingana na thamani ya bidhaa alizonunua. Hapo suala la dai/toa risiti halipo ni 'otomatiki' hakuna kusumbuana.

Kwenye biashara za mitaani, na maeneo mengine zenye mikusanyiko mikubwa ya wajasiriamali na wateja wengi kama, Kariakoo, Mbagala-Rangitatu, Mbezi-Luis, Manzese, Mwenge, Tegeta, Gongolamboto, Chanija nakadhalika, matumizi ya utaratibu kama huo si kwa viwango tarajiwa.

Waliyo na EFD wachache, utaratibu wa kudai risiti ni keromno hadi kununiana. Tatizo ni kukwepa VAT muuazaji akisema usipodai risiti bei ni kiasi fulani ukidai risiti ni kiasi fulani, mteja atakubali kulipa bila risiti.

Tusidanganyane, kwa asilimia 18 VAT inayotozwa uzalendo haupo.

Ikipungua kwa kiwango ambacho kitawafanya Watanzania kuwa wazalendo haina shida hata wauzaji watapata bidhaa kwa gharama nafuu; muuzaji na mteja tutapata risiti bila vikwazo.

Vilevile, tutasema 'watumishi wa TRA ni wenye ukwasi' hata kama mishahara yao ni mikubwa, tukumbuke ni binadamu wenye udhaifu kama wengine. Shetani, amejikita kwenye rasilimali-fedha pia dunia imezingirwa na bidhaa nyingi, hatarishi/tamanishi kupindukia .

Bila kuimarisha mifumo ya kielekitroniki, pamoja na sera, sheria na kusimamia ipasavyo; Serikali itaendela kupoteza fedha nyingi hata kama kutakuwepo na miamala husika.

Matumizi ya kielekitroniki pamoja na miamala kupitia mashine zinazotumiwa na binadamu, ni rahisi kughushiwa.

Wataalamu husika, kwa ujanja wa kiibilisi wanao uwezo wa kutoa 'miamala batili' yenye kuwanufaisha wachache badala ya wengi maana miamala husika haitawasilisha fedha Hazina.

Kwa msemo wa mitaani: fedha ya umma inapigwa kiwiko" pia inachukua muda mrefu kugundua udanganyifu husika. Hivyo, hasara inakuwa kubwa kiasi cha kuzorotesha huduma za kijamii na maendeleo tarajiwa.

Serikali iwe macho sana kuhusu matumizi ya kielekitroni, na panapogundulika ubadhilifu, hatua kali kiutawala na kisheria zichukuliwe bila kukawia na kwa misingi ya uwajibikaji.



Trump na Biden kwenye mdahalo

# Ni mdahalo ama shambulizi?

Inatoka uk. 14

**SHAMBULIO DHIDI YA TRUMP**

Marekani inarejea wakati wa giza? Hilo linaweza kuwa swali la msingi kwa wanaoangalia mwenendo wa kisiasa wa taifa hilo hasa hivi karibuni au ndani ya muda wa mchakato wa utafutaji wa wagombea.

Katika historia ya Marekani, zaidi ya nusu karne iliyopita, ndugu wawili wa Kennedy, mmoja akiwa rais na mmoja mgombea urais, waliuawa kwa risasi za wadunguaji wakiwa kwenye mazingira kama ilivyokuwa kwa Trump.

Pia katika patashika hizo za kisiasa viongozi wa haki za kiraia kama vile Medgar Evers, Martin Luther King Jr na Malcolm X wote pia walipoteza maisha yao katika ghasia za kisiasa. Tumekumbuka historia kwa sababu almanusura historia ya Marekani ibadilike kama ilivyokuwa miaka ya 1960 baada ya risasi ambayo inaonekana ilidhamiria kumuondoa uhai Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump kukwaruza sikio lake na kwenda kumuua mtu mwingine!

Haikuwa risasi moja iliyopigwa kuelekea alipo rais huyo wa zamani, mdunguaji akiwa juu la paa aliachia risasi kadhaa kabla ya kumalizwa na wadunguaji wa serikali waliokuwa wanamlinda rais huyo wa zamani.

Tukio hili la Pennsylvania la Jumamosi Julai 13 usiku linaonekana kuanza kuwafanya watu wajiulize kuhusu kile kinachoonekana kuparaganyika kwa masuala ya usalama ya Marekani.

Tukio hili linakumbusha kupigwa risasi kwa Ronald Reagan kitendo kilichofanywa na John Hinkley Jr mwaka 1981. Ingawa wachambuzi wa mambo wanasema ni ngumu kutabiri athari ya tukio hilo la Jumamosi, Wamarekani sasa wanahitaji umoja wa kitaifa zaidi kuliko kipindi chochote kwa kuangalia mwenendo wa siasa wa sasa wa Marekani.

Saa chache baada ya tukio hilo, Rais Joe Biden, aliyekuwa mpinzani mkubwa wa Trump katika kinyang'anyiro cha Novemba, alizungumza na waandishi wa habari mjini Delaware na kulaani kitendo hicho.

"Aina hii ya vurugu haikubaliki Marekani," alisema na kuongeza. "Hatuwezi kuwa hivi. Hatuwezi kuunga mkono jambo hili."

Rais huyo baadaye alizungumza kwa njia ya simu na rais huyo wa zamani na kumpa pole.

Baadhi ya wanasiasa wa Chama cha Republican wamelaumu shambulio hilo na kutumia maneno makali kuhusu shambulio huku wakilihusisha na Chama cha Democratic ambao wamedai wanamhofia mgombea huyu wa Republican.

Wanadai kuwa, msingi mkuu wa kampeni ya Biden ni kwamba, Donald Trump ni fashisti!

Kuna wanaoamini kwamba jaribio hilo la kumuua Trump limemwongezea mvuto na watu wengi kimuunga mkono.

**HUYU NDIYE BI. HARRIS**

Kamala Harris aliandika historia ya kuwa mwanamke wa kwanza mweusi na mwenye asili ya Asia kuhudumu kama makamu wa rais.

Uongozi wake kama makamu wa rais unakumbukwa na wafuasi wake kwa utetezi wake wa haki za uzazi.

Hakuna shaka kwamba ana mvuto kwa wapiga kura weusi na historia yake kama mwendesha mashtaka machachari ni vitu vinavyombeba.

Miaka mitano tu iliyopita, Bi. Harris alikuwa seneta kutoka California akitarajia kushinda uteuzi wa chama cha Demokrati kuwa rais.

Alianza kazi yake katika Ofisi ya Mwanasheria wa Wilaya ya Alameda na kuwa wakili wa wilaya na kisha mwendesha mashtaka mkuu wa San Francisco mnamo 2003, kabla ya kuchaguliwa kuwa mwanamke wa kwanza mweusi kuhudumu kama mwanasheria mkuu wa California, wakili mkuu na afisa wa utekelezaji wa sheria katika jimbo lenye watu wengi zaidi Marekani.

Alipata sifa kama mmoja wa nyota wanaochipukia wa chama cha Demokrati akitumia kasi hiyo kumsukuma kuchaguliwa kama seneta mdogo wa California mwaka wa 2017.

Lakini malengo yake ya urais hayakufaulu mnamo 2020 lakini akaukwaa umakamu.

Ni mzaliwa wa Oakland, California, kwa wazazi wawili wahamiaji; mama mzaliwa wa India na baba mzaliwa wa Jamaica. Wazazi wake walitalikiana akiwa na umri wa miaka mitano na alilelewa hasa na mama yake Mhindu, Shyamala Gopalan Harris, mtafiti wa saratani na mwanaharakati wa haki za kiraia.

Alikua akijishughulisha na urithi wake wa Kihindi, akiungana na mamake kutembelea India, lakini Bi Harris amesema kwamba mamake alikubali utamaduni wa watu weusi wa Oakland, akiwazamisha 'mazima' binti zake wawili - Kamala na dadake mdogo Maya - ndani ya utamaduni huo.

Je, atapitishwa rasmi na Demokrati? Akipitishwa, atamshinda Trump? Ni jambo la kusubiri.

# Maporomoko yaua watu 157 Ethiopia

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

WATU 157 wamefariki dunia kutokana na maporomoko ya ardhi Kusini mwa Ethiopia,maafisa wa eneo hilo wamesema.

Matukio mawili yanakisiwa kutokea juzi jioni na jana asubuhi, baada ya mvua kubwa kunyesha katika eneo la mbali la milima la ukanda wa Gofa.

Mamlaka ya eneo hilo ilisema kuwa utafutaji wa manusura ulikuwa unaendelea, lakini idadi ya vifo bado inaweza kuongezeka.

Picha zilionyesha mamia ya watu wakiwa wamekusanyika kwenye eneo la tukio na wengine wakichimba chini ya vifusi kutafuta watu walionasa.

Meskir Mitku, Msimamizi Mkuu wa eneo la Gofa, alisema wanawake, watoto na maafisa wa polisi, walikuwa miongoni mwa waliopoteza maisha.

"Kulikuwa na mvua kubwa siku ya Jumapili usiku na baadhi ya watu walifariki dunia kutokana na maporomoko ya ardhi," Msemaji wa Serikali wa Wilaya ya Gofa, Kassahun Abayneh, alisema.

Gofa ni sehemu ya jimbo linalojulikana kama Kusini mwa Ethiopia, lililoko karibu kilomita 320 Kusini-Magharibi mwa Mji Mkuu, Addis Ababa.

Kusini mwa Ethiopia, ni miongoni mwa maeneo ya nchi hiyo ambayo yamekumbwa na mvua kubwa na mafuriko katika miezi ya hivi karibuni, kulingana na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (Ocha).

Lakini matukio ya maporomoko ya ardhi na mafuriko, yamekuwa yakitokea siku za nyuma.

Mei, 2016, takriban watu 50 waliuawa katika mafuriko na maporomoko ya ardhi kufuatia mvua kubwa kusini mwa nchi. BBC.





# Israel yaanzisha operesheni kubwa Khan Yunis

**YERUSALEM, Israel**

ISRAEL ilitangaza Jumatatu iliyopita kuuawa kwa mateka wake wawili waliokuwa wameshikiliwa huko Gaza, na jeshi lilisema katika taarifa tofauti kwamba Hamas inahifadhi miili hiyo na kwamba inafanya uchunguzi kuhusu mazingira ya vifo vyao.

Jukwaa la familia za mateka waliozuiliwa lilisema katika taarifa kwamba Yagiv Buchstab (35) na Alex Dansig (76), walitekwa nyara wakati wa shambulio la Oktoba 7, mwaka huu ambalo lilifanywa na Hamas ndani ya Israel na kwamba mauaji yao yanawakilisha ukumbusho wa hitaji la dharura la kuwarudisha mateka wote nyumbani kwa mujibu wa Shirika la Habari la Ufaransa Agence France-Presse.

Haya yanajiri huku Jeshi la Israel likiwataka Wapalestina kuhama vitongoji vya Mashariki mwa mji wa Khan Yunis, Kusini mwa Ukanda wa Gaza na kuelekea katika eneo la Al-Mawasi kwa ajili ya kujiandaa kuanzisha kile ilichoeleza kuwa ni operesheni kubwa kujibu shughuli za silaha zinazofanywa katika eneo hilo.

Jeshi limesema katika taarifa yake kwamba makombora yalirushwa kuelekea Israel kutoka huko, na kwamba eneo hili ni miongoni mwa maeneo yanayoitwa ya kibinadamu ambayo Israel iliwataka Wapalestina waliokimbia makazi yao kuhamia. BBC.

# Wanasiasa watatu wa upinzani Uganda mbaroni



**KAMPALA, Uganda**

WANASIASA watatu wa upinzani nchini Uganda, wamewekwa rumande usiku wa kuamkia maandamano yaliyopigwa marufuku dhidi ya ufisadi, polisi walisema juzi huku Kiongozi wa Upinzani, Bobi Wine akisema kuwa vikosi vya usalama vilivyojihami, vilikuwa vinazingira makao makuu ya chama chake.

Hatua hiyo inajiri siku mbili baada ya Rais Yoweri Museveni, aliyetawala nchi hiyo kwa takriban miongo minne, kuonya kwamba Waganda waliopanga kuingia mitaani jana Jumanne, wanacheza na moto.

Wabunge watatu na watu wengine saba, walifikishwa mahakamani jana wakishtakiwa kwa makosa mbalimbali na kurudishwa gerezani, Msemaji wa Polisi wa Uganda, Kituuma Rusoke aliiambia AFP juzi bila kutoa maelezo zaidi kuhusu mashitaka yanayowakabili wanasiasa na watu hao.

VOA.



# 11 mbaroni kwa tuhuma za uhaini

**FREETOWN, Sierra Leone**

MAHAKAMA ya Sierra Leone, juzi Jumatatu iliwatia hatiani watu 11 kwa uhaini na makosa mengine kuhusiana na kile serikali inakiita jaribio la mapinduzi Novemba, mwaka jana, Msemaji wa Mahakama amesema.

Amadu Koita Makalo, mwanajeshi wa zamani na mlinzi wa Rais wa zamani Ernest Bai Koroma, amehukumiwa miaka 182 gerezani kwa makosa ya uhaini, mauaji na kumpiga risasi kwa nia ya kumuua, Elkass Sannoh, Mkuu wa Mawasiliano wa Mahakama ameiambia AFP.

Koita Makalo alifuatiliwa sana kwenye mitandao ya kijamii ambapo aliikosoa serikali ya Rais wa sasa, Julius Maada Bio, huku serikali hapo awali ikimtaja kuwa ni mmoja wa wanaopanga njama za mapinduzi.

Wengine 10 pia walikutwa na hatia ya uhaini na mauaji, lakini haikueleza urefu wa vifungo vyao kwa kuwa hati ya mahakama ilikuwa haijatolewa.

Novemba 26, mwaka jana, watu wenye silaha walivamia kambi mbili za jeshi, magereza mawili na vituo viwili vya polisi kujaribu mapinduzi. VOA.

# Wajumbe wengi wa Democrat wamuunga mkono Harris

**WASHINGTON, Marekani**

MAKAMU wa Rais, Kamala Harris, amepata uungwaji mkono wa wajumbe wa kutosha wa chama cha Democratic kuwa mteule wa chama hicho kuwa Rais, mshirika wa BBC wa Marekani CBS News anaripoti.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Habari la Associated Press juzi Jumatatu jioni ulisema Harris amepokea uungwaji mkono wa zaidi ya wajumbe 1,976 wanaohitajika kushinda uteuzi katika duru la kwanza la upigaji kura.

Wajumbe ni watu ambao wamechaguliwa kuwakilisha eneo lao la uchaguzi katika Kongamano la Kitaifa la Kidemokrasia (DNC), tukio kuu la uteuzi wa chama.

Uidhinishaji kama huo siyo rasmi kisheria, lakini ikiwa jumla wajumbe wataendelea kumuunga mkono kati ya sasa na wakati wajumbe watakapopiga kura zao, zilizopangwa kufanyika kuanzia Agosti mosi hadi 7, mwaka huu, Harris atashinda rasmi uteuzi wa chama.

Wajumbe kutoka angalau majimbo 27, wametoa taarifa za wajumbe wao kamili wanaomuunga mkono Harris, kwa mujibu wa CBS.

Utafiti huo ni dalili ya msingi ya kumuunga mkono Harris baada ya Rais Joe Biden, kujiondoa katika kinyang'anyiro siku ya Jumapil iliyopita.

BBC.



# Zengekala; Mwimbaji aliyetingisha medani ya burudani

## ● Alituachia Msamiati wa neno 'Solemba' unaotumika mpaka sasa



**Na Mwandishi Maalumu**

DISEMBA 17 mwaka 1987, wingu zito la huzuni likiigubika anga ya Tanzania baada ya aliyekuwa mmoja wa wanamuziki bora kabisa katika muziki wa dansi kuwahi kutokea katika ukanda wa Afrika Mashariki, Nico Zengekala kufariki dunia.

Taarifa za kifo cha mwanamuziki huyo ambaye ndiyo kwanza alikuwa kijana mdogo mwenye umri wa miaka 24 tu, ziliwashtua watu wengi na kuwahuzunisha sana kutokana na kijana huyo ndiyo kwanza kiukweli alikuwa ameanza kula mafanikio ya kipaji chake adhimu alichojaaliwa.

Nico alifikwa na umauti akiwa ndani nyumbani kwake Mtaa wa Sikukuu, jijini Dar es salaam, katika nyumba ambazo zilikuwa zikimilikiwa na iliyokuwa Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA) ambayo ndiyo ilikuwa mwajiri wake kupitia bendi yake ya Muziki wa dansi ya Juwata Jazz band aliyeitumikia kwa miaka miwili tu.

Kwa mujibu wa ripoti ya madaktari, chanzo cha kifo cha mwanamuziki huyo aliyekuwa na ulemavu wa macho (Kipofu) kilitokana na shambulio la maradhi ya ugonjwa wa kuanguka maarufu kama Kifafa ambayo 'yalimpiga' na kuyagharimu maisha yake katika umri wake mdogo mno tofauti kabisa na umaarufu wake.

Mwanamuziki huyu ambaye alikuwa ni raia wa Kenya, aliingia nchini mwaka 1982 akitokea bendi maarufu ya Les Quban iliyokuwa nchini Kenya ambayo pia ilikuwa na mwanamuziki nyota kutoka nchini Tanzania Juma Kilaza pamoja na nyota mwingine aliyekuwa mpuliza Saxophone maarufu, Comson Mkomwa.

Nyota ya Zengekala katika bendi ya Les Quban ilikuwa iking'arishwa pia na wanamuziki mahiri wa bendi hiyo kama Mohamed Tungwa aliyekuwa akipiga kitaa la Solo, Said Makelele na Jumanne Mwamzungu waliokuwa wakipuliza Ala za Upepo, pamoja na nyota wengine Shaibu Monduli, Majuto Mbungani nk.

Bendi hiyo iliyoamua kuhamishia shughuli zake za kimuziki nchini Tanzania kutoka huko nchini Kenya ilileta ushindani mkubwa baada ya kutoa vibao kadhaa vilivyoipa umaarufu mkubwa kama 'Mtoto Jackie', 'Kambarage', 'Shemango' na nyinginezo, huku sauti ya Zengekala ikionekana kuwa mwiba mchungu kwa bendi nyingi za muziki wa dansi nchini.

Kutokana na nyota ya mwanamuziki huyo kung'aa sana katika bendi yake ya Les Quban, uongozi wa bendi ya Juwata Jazz Band (JJB) uliamua kumpelekea 'Ofa' ya kumuomba mwanamuziki huyo kujiunga na bendi yao, naye bila hiana akashindwa kukataa kutokana na mapenzi makubwa aliyekuwa nayo kwa bendi ya Juwata ambayo alieleza kuwa ilikuwa ni moja ya ndoto zake kubwa kuimbia bendi hiyo.

Kuingia kwa mwanamuziki huyo katika bendi ya Juwata (Msondo Ngoma) kulimfanya azidi kuwa bora zaidi kutokana na kukutana na 'vichwa' vingine mahiri katika uimbaji kama Joseph Lusungu, Khamis Kitambi, Tx Moshi William, Suleiman Mwembwe, Shaaban Dede, Tino Masenge 'Arawa' (wote hao nao wametangulia mbele ya haki), na wengineo wengi.

Akiwa ndiyo kwanza ameingia ndani ya Juwata, Zengekela alianza kuonesha makali yake na kutishia kuwafunika baadhi ya nyota kadhaa aliowakuta ndani ya bendi hiyo kutokana na sauti yake tamu na ya kipekee.

Kibao kama 'Priscilla' ambacho aliimba kwa hisia kali akipokezana na Suleiman Mbwembwe kilikuwa tishio na kuzidi kumpaisha kupita maelezo, lakini funga kazi kabisa ulikuwa ni utunzi wake wa wimbo 'Solemba'.

Solemba ni jina la msichana aliyetokea kupendwa mno na mwanamuziki Zengekala lakini msichana huyo anaelezwa katika wimbo huo kuwa hakuwa na mapenzi ya kweli na Nico kiasi cha kumfanyia vituko kadhaa vyenye kumvunja moyo na kumuumiza sana mwanamuziki huyo.

Kituko cha kumsubirisha (kumgandisha) mwanamuziki huyo kuanzia asubuhi mpaka saa nane mchana huku akingojea kama atatokea kama ambavyo alimuahidi kulitosha kabisa kutoa msamiati mpya wa lugha ya Kiswahili kuhusu tukio hilo, na hivyo kitendo hicho cha kumuacha mtu akikusubiri bila kutokea kubatizwa jina la 'Solemba'.

Mwanamuziki Ruta Bushoke, katika wimbo maarufu alioshirikishwa na mwanamuziki wa Uganda Juliana Kanyomozi uitwao 'Usiende Mbali nami', ameimba mara kadhaa akisisitiza kwa kumsihi msichana asije 'Kumuacha Solemba' akimaanisha msichana huyo asije kushindwa kutokea kwenye miadi yao.


Hivi ndivyo namna Kiswahili kilivyolazimika kurithi neno 'Solemba' kutoka kwenye utunzi wa mwanamuziki Nico Zengekela na kuliingiza kwenye msamiati wa matumizi yake na hivyo mwanamuziki huyo kuacha 'Legacy' katika moja ya tungo zake nzuri mno kuwahi kutungwa naye katika maisha yake mafupi ya muziki duniani.

Marehemu Nico Zengekala alizikwa kijijini kwao siku ya Disemba 24, mwaka 1987 huko Mwatate Voi, Taita Mjini Mombasa nchini Kenya.

Mungu azidi kumpumzisha kwa Amani.

Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.

**Bendi hiyo iliyoamua kuhamishia shughuli zake za kimuziki nchini Tanzania kutoka huko nchini Kenya ilileta ushindani mkubwa baada ya kutoa vibao kadhaa vilivyoipa umaarufu mkubwa kama 'Mtoto Jackie', 'Kambarage', 'Shemango' na nyinginezo, huku sauti ya Zengekala ikionekana kuwa mwiba mchungu kwa bendi nyingi za muziki wa dansi nchini.**



# Kuna cha kujifunza Kombe la Kagame




**Na Hamid Yassin**

MICHUANO ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama Kombe la Kagame 2024 ilifikia tamati Jumapili wiki hii kwa timu ya Red Arrows ya Zambia kutwaa ubingwa kwa kuifunga APR ya Rwanda kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 10-9 baada ya timu hizo kwenda sare ya bao 1-1 kwa dakika 120 za mchezo huo.

Fainali hiyo ya 47 ya michuano hiyo ya Kagame ilizikutanisha timu hizo huku APR ya Rwanda ilikuwa ikisaka taji la nne la michuano hiyo dhidi ya waalikwa hao kutoka Red Arrows.

Timu hizo zimefuzu hatua hiyo baada ya kushinda mechi za nusu fainali, APR ikiizima Al Hilal ya Sudan kwa penalti 5-4 baada ya dakika 120 kumalizika bila ya bao lolote, huku Wazambia wakitumia dakika 30 za nyongeza kuwafumua Al Wadi pia ya Sudan kwa mabao 2-0.

Hii ilikuwa ni fainali za tisa kwa Wanyarwanda katika michuano hii iliyopewa jina la Kagame Cup kuanzia mwaka 2002 baada ya Rais wa Rwanda, Paul Kagame kujitosa kuidhamini.

APR ilishacheza awali fainali nane tofauti, tatu ikifanikiwa kutwaa ubingwa mwaka 2004, 2007 na 2010, huku ikipoteza nyingine tano za mwaka 1996, 2000, 2005, 2023 na 2014.

Kwa Maafande wa Red Arrows kutoka Zambia walioshiriki kama timu mwalikwa, hizi ni fainali za kwanza za michuano hiyo ya Kagame, na ilipenya hatua ya nusu fainali ikiwa kama mshindwa bora (best looser) kutokea Kundi B.

Red Arrows ilimaliza nafasi ya pili kwa kuvuna pointi sita katika mechi tatu, nyuma ya vinara Al Hilal iliyomaliza na pointi tisa ikiwa timu pekee iliyoshinda mechi zote tatu za makundi ya michuano hiyo iliyoanza Julai 9 ikishirikisha timu 12 na kuchezwa kwenye viwanja viwili vya KMC uliopo Mwenge na Azam Complex, Chamazi vyote vya jijini Dar es Salaam.

### AZAM, SIMBA NA YANGA KUJITOA

Timu za Simba, Yanga na Azam FC walilitaarifu Baraza la Soka kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) kuwa hawatoweza kushiriki mashindano haya ya Kagame kutokana na ratiba kutokuwa rafiki kwao.

Simba, Yanga na Azam zilisema kuwa, zilipanga kufanya maandalizi ya msimu mpya 'Pre Season' nje ya Tanzania na walishapanga ratiba zao na nchi watakazokwenda kujiandaa.

Ingawa Rais wa CECAFA, Wallace Karia alikaririwa akisema kuwa, hakukuwa na mapungufu yoyote kwa kukosekana kwa vigogo hivyo vilivyopaswa kuwa wenyeji wa michuano hiyo, lakini ukweli ulio wazi yalikosa msisimko mkubwa kwa kutokuwepo kwa timu hizo pendwa.

Siyo msisimko tu, hata suala la kukosa mapato kwa michuano hii imekuwa ni pigo kubwa kwa CECAFA ambayo imeingia gharama kubwa kuyaandaa na kuzihudumia timu zote shiriki kwa wiki mbili mfululizo.

Pamoja na kupata udhamini wa Rais Kagame wa Rwanda na Shirika za Bandari la hapa nchini, bado CECAFA ingeweza kupata fedha zaidi kama Simba na Yanga wangeshiriki michuano hiyo.

Rais Kagame tangu aanze kudhamini michuano hii mwaka 2002 amekuwa akitoa fedha za zawadi tu ambazo ni dola 30, 000 huku gharama nyingine kama za maradhi, chakula na usafiri wa ndani kwa timu zote unabaki mikononi mwa CECAFA yenyewe.

Pia hii inakuwa mara ya kwanza kwa michuano hii kufanyika Tanzania huku timu zake zote kubwa zikikosa kushiriki kutokana na changamoto ya ratiba ya michuano hiyo.

### CHANGAMOTO YA RATIBA NA ZAWADI

Huko nyuma michuano hii ya Kombe la Kagame ilikuwa inafanyika kati ya mwezi Januari na Februari, lakini kutokana na mabadiliko ya kuanza kwa misimu ya michuano kwa nchi nyingi za Afrika zikiwemo za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati kutoka mwanzoni mwa mwaka hadi katikati ya mwaka, hata michuano hii nayo ikaanza kuteteleka.

Mara kadhaa imeshindwa kufanyika aidha kwa kuingiliana na michuano mingine ya nchi wanachama ama kukosekana kwa wadhamini wa kuyafadhili.

Mfadhili pekee wa uhakika kwa miaka 22 sasa ni Rais Kagame ambaye anatoa zawadi za washindi wa mashindano pekee. Ambapo bingwa hujipatia dola 20,000 na mshindi wa pili huondoka na dola 7,000 na yule wa tatu huambulia dola 3,000.

Miaka hiyo ya nyuma fedha hizi kwa timu za Tanzania zilikuwa nyingi sana kutokana na ukata uliokuwa unawakabili, hivyo haikuhitaji nguvu kubwa kuzishawishi kushiriki michuano hii, lakini siku hizi timu hizi zina ukwasi mkubwa wa kuweza kudengulia kiasi cha dola 30,000 za zawadi kwa washindi.

Timu zote tatu kubwa za Tanzania zilizojitoa kwenye mashindano haya hivi sasa ziko nje ya nchi kwenye kambi za maandalizi ya msimu mpya. Simba hipo Ismailia Misri, Azam FC wapo Morocco na Yanga ipo Afrika Kusini!

Ebu fikiri zinatumia kiasi gani cha fedha kwa kambi hizo za nje ya nchi za wastani waa wiki tatu zinazohusisha zaidi ya watu 40 kwa kila timu? Huko nyuma timu hizi zilikuwa zinashindwa hata kuweka kambi hapa hapa nchini na wachezaji walikuwa wanatokea nyumbani kwenda mazoezini!

Hivi leo unaweza kuzishawishi kirahisi kushiriki michuano ya wiki mbili kwa dau la dola 30,000 ambazo ni sawa na fedha za Tanzania shilingi milioni 75? Simba na Yanga hivi sasa zikicheza mechi moja kubwa kama zile za Simba Day na Siku ya Wananchi wanaingiza zaidi ya shilingi milioni 400 baada ya makato ya Serikali, Uwanja na TFF!

Umefika wakati sasa CECAFA kukaa na nchi wanachama kutathimini michuano hii hususani katika masuala ya muda mwafaka wa kufanyika na zawadi kwa washindi, ingawa Rais wake, Karia anasema huu ndiyo muda sahihi wa kufanyika.

Michuano hii ilikuwa ishirikishe timu shiriki 16, ambapo timu 12 zilipaswa kutoka miongoni mwa nchi wanachama huku nne zikitoka kwa nchi zilizopata mwaliko, lakini timu kadhaa zilijitoa zikiwemo Azam FC, Simba, Yanga, TP Mazembe ya Congo DR na Big Nyasa Bullets ya Malawi.

Wanachama wa CECAFA ni Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi, Sudani, Eritrea, Zanzibar, Sudan Kusini, Somalia na Djibouti.

# Chelsea kutumia makinda kurudisha heshima EPL





**Na Valensi Mbaga**

KLABU ya Chelsea imeendelea kutekeleza mpango wake wa kusuka kikosi chenye ushindani kwa kutumia vijana wadogo na kurudisha utawala wao wa kisoka uliopotea takribani misimu miwili iliyopita.

Japo tayari wameshakamilisha usajili wa nyota kama Renato Vega kutokea kule Brazil, Tosin kutoka Fulham na kwa sasa mmoja wa wachezaji makinda machachari zaidi wanaotajwa kuangaziwa kwa sasa ni Gabriel Mec, ambaye amezivutia timu kadhaa za Ligi Kuu, zikiwemo timu hiyo, Manchester United na Aston Villa.

Jina lake kamili ni Gabriel Ferreira de Carvalho maarufu kama Gabriel Mec, ni nyota kinda wa akademi ya Gremio na kwa mujibu wa taarifa ni kwamba viongozi wawili wa Chelsea wameonekana wakiwa karibu na baba wa nyota huyo mwenye miaka 16 anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji huku taarifa zikisema Chelsea inataka kumsajili kinda huyo anayetabiriwa makubwa.

Gabriel Mec ni mwanasoka mchanga na mwenye kipaji, amekuwa akifanya mambo makubwa katika duru za soka kutokana na uchezaji wake wa kuvutia na uwezo wake.

Gabriel Mec, anayejulikana kwa umahiri wake wa kiufundi na uelewa wa kimbinu wa mchezo, amekuwa kwenye rada za maskauti kwa muda sasa. Uwezo wake wa kucheza katika nafasi tofauti katika safu ya kiungo na ulinzi unamfanya kuwa nyenzo muhimu kwa timu yoyote inayotaka kuongeza kina na ubora kwenye orodha yao.

Chelsea, chini ya uongozi wa Meneja wao mpya Enzo Maresca na timu ya usimamizi, wameripotiwa kuanzisha majadiliano kupata huduma za Gabriel Mec. Klabu hiyo ya London, inayojulikana kwa kusajili kimkakati kwa vipaji vya vijana wenye uwezo wa kukua, inaona Mec kama mchezaji ambaye anaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yao ya baadaye.

Hata hivyo, Chelsea hawako peke yao katika harakati zao za kumnasa Gabriel Mec. Klabu ya Manchester United yenye historia nzuri na yenye mvuto wa kukuza vipaji vya vijana, pia imeonyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo. Kwa msisitizo wao wa kuchanganya vijana na uzoefu, Manchester United wanamuona Mec kama mchezaji ambaye anaweza kufaa katika mipango yao ya muda mrefu.

Aston Villa ni klabu nyingine inayojulikana kwa uwekezaji wao wa hivi majuzi katika wachezaji wa kutumainiwa, imetupa kofia yao ulingoni pia. Klabu ya Midlands, inayotaka kuendeleza uchezaji wao wa hivi majuzi na kujiimarisha zaidi katika ligi ya daraja la kwanza, inamwona Gabriel Mec kama kiungo muhimu katika kikosi chao.

Kumtafuta Gabriel Mec kunadhihirisha hali ya ushindani wa soko la uhamisho, hasa katika Ligi ya kuu ya England ambapo vilabu vinatazamia kupata makali ya ushindani. Mazungumzo na majadiliano yanatarajiwa kuimarika huku kila klabu ikishindana kupata saini ya Mec.

Kwa Gabriel Mec mwenyewe, nia kutoka kwa vilabu vingi vya juu huwasilisha mchakato muhimu wa kufanya maamuzi. Mambo kama vile muda wa kucheza, fursa za maendeleo, na mradi wa jumla wa klabu itakuwa na uzito mkubwa katika uamuzi wake anapozingatia uhamisho wake ujao wa kazi.

Kwa kumalizia, nia ya Chelsea, Manchester United, na Aston Villa katika Gabriel Mec inaangazia mustakabali mzuri ulio mbele kwa mwanasoka huyo mwenye kipawa. Wakati majadiliano na mazungumzo yakiendelea, inabakia kuonekana ni klabu gani itafanikiwa kupata huduma yake na jinsi Gabriel Mec atakavyochangia katika hali ya mabadiliko ya Ligi Kuu katika misimu ijayo. Tutegemee kumuona akifanya makubwa na kuwa miongoni mwa wanasoka bora wa kizazi cha hivi sasa.



## Kona ya Urembo



**Na Unosye Atufigwege**

# Aina za ngozi, changamoto zake na sifa zake kiafya

BAADA ya kujua namna bora za kutunza ngozi, leo ingependeza kama ukijua aina gani ambayo muonekano wa ngozi yako pengine inadondokea humo.

Kwa kuangazia aina za ngozi ni muhimu kujua aina ya ngozi uliyokuwa nayo kabla ya kuanza safari ya kutibu au kutunza ngozi yako.

Kuna aina kuu tano za ngozi ambazo ni ngozi kavu (dry skin), ya mafuta (oily skin), mchanganyiko (combination skin), ya kawaida (normal skin) pamoja na sensitive skin (ngozi nyeti/dhaifu).



Ngozi ya kawaida

**SIFA ZA NGOZI NA JINSI YA KUKABILIANA NAZO**

**1. Ngozi ya kawaida**

Ngozi hii sio kavu sana na sio mafuta sana. Ina muonekano wa kawaida, hakuna kasoro na huonekana safi, laini na hauhitaji huduma maalum zaidi tu ya kufanya uangalifu wa hali ya kawaida ya ngozi ili kuendelea kuilinda. Yaani kwa kifupi ni ngozi isiyo na heka heka.

Epuka sana kutumia bidhaa zenye viambata sumu kama vile Hydroquinone, mercury, steroid, paraben, silicone na nyinginezo kwani vinaweza kuharibu ulinzi ambao ngozi yako ipo nayo (Skin barrier), bila kusahau matumizi sahihi ya sun screen.

**2. Ngozi kavu**

Hii ni aina ya ngozi ambayo mtu anapata ukavu katika ngozi yake na mara nyingi huambatana na kupauka au kukosa nuru na muda mwingine kupasuka au kuweka nyufa ndogondogo au kuwa kama umepaka poda au jivu.

Jinsi ya kukabiliana na ngozi hii ni kuhakikisha unatumia bidhaa zitakazo ongeza unyevu na kuondoa hali ya ukavu katika ngozi; mfano ni bidhaa zenye viambata kama vile hyaluronic acid, lactic acid, vitamin E, cocoa butter, shea butter, pamoja na bidhaa zenye kuboresha ulinzi wa ngozi.

Kwa umuhimu kama una ngozi kavu epuka kutumia bidhaa zitakazokausha mafuta katika ngozi yako kwani utazidisha ukavu katika ngozi yako na ngozi yako itazeeka haraka kabla ya wakati wake.



Ngozi kavu

**3. Ngozi ya mafuta**

Hii ni aina ya ngozi ambayo mtu anakuwa na mafuta hata kama hajapaka mafuta hii hutokana na mwili kuweza kutengeneza mafuta yake kupita kiasi.

Aina hii ya ngozi huambatana na uwepo wa chunusi au rashes katika ngozi na kuongezeka size ya vitundu vya ngozi (enlarged pores).

Oil skin huweza kudhibitiwa kwa kutumia bidhaa zenye kudhibiti kiwango cha uzalishwaji wa mafuta katika ngozi na kudhibiti size ya tundu ya ngozi.

Aina hii ya ngozi hujulikana pia kama Acne prone skin (yaani ngozi yenye kukabiliwa na tatizo la chunusi mara kwa mara), hivyo kama una ngozi ya aina hii jitahidi kutumia light weight na oil free products yaani bidhaa ambazo ni nyepesi (gel type) na zisizo na mafuta kwa sababu ngozi yako tayari inazalisha mafuta ya kutosha na hata ziada na kupelekea kuziba kwa vitundu vya ngozi na kuzaliana kwa bacteria katika matundu ya ngozi na hivyo kusababisha chunusi.



Ngozi ya mafuta

**4. Ngozi mchanganyiko**

Hii ni aina ya ngozi ambayo mtu anaweza kuwa na mafuta kwa baadhi ya sehemu na baadhi ya maeneo kuwa na ukavu.

Mfano katika ngozi ya uso mtu anaweza kuwa na ukavu katika maeneo ya mashavu mpaka kwenye taya na akawa na mafuta kwenye T-zone (paji la uso, puani na kidevuni).

Aina hii ya ngozi ni ngumu kidogo kukabiliana nayo hivyo mwenye ngozi hii anashauriwa zaidi kutumia bidhaa ambazo zitasaidia kutokuleta ukavu maeneo yalio makavu na kutokuzidisha mafuta maeneo yenye mafuta.

**5. Ngozi nyeti/dhaifu**

Hii ni aina ya ngozi ambayo inapata miwasho, wekundu, kuwaka moto na hata rashes. Aina hii ya ngozi inakuwa imekosa kizuizi (au kinga) na kuifanya iwe rahisi kwa vijidudu kuingia ndani yake na kuongeza uwezekano wa kuwa na maambukizi au mzio.

Hali hii inaweza kusababishwa na ngozi kushinda kuzoea baridi, kipupwe, matumizi ya vipodozi vikali, mabadiliko ya haraka ya homoni hususani kwa wanawake, mzio wa baadhi ya vyakula au viungo (kuna watu wakila samaki fulani, mayai, maziwa, karanga nwanadhurika ).

Hivyo ni vyema mtu ukafahamu kama upo na mzio wowote.

Kama una aina hii ya ngozi inashauriwa sana kuwa makini katika nini utumie na kipi usitumie ili kukabiliana nayo.

Ngozi yako inaweza kuwa katika moja ya makundi tajwa hapo juu na bado ikawa ni dhaifu hivyo ni vema kuitambua na pia utumie bidhaa ambazo ni maalumu kwa watu wenye ngozi dhaifu.

Kumbuka aina ya ngozi yako.

> **Epuka sana kutumia bidhaa zenye viambata sumu kama vile Hydroquinone, mercury, steroid, paraben, silicone na nyinginezo kwani vinaweza kuharibu ulinzi ambao ngozi yako ipo nayo (Skin barrier), bila kusahau matumizi sahihi ya sun screen.**



Ngozi ya nyeti

MANCHESTER, England

# De Bruyne anabaki Man City

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema kiungo mshambuliaji wa timu yake, Kevin De Bruyne hana mpango wa kuhamia Saudi Arabia kama inavyodaiwa kuwa anawaniwa na Klabu ya Al-Ittihad inayoshiki Saudi Pro League

Guardiola amesema; "Kama kuna mtu anaondoka tutazungumza kuhusu hilo, ubora wa Wachezaji tulionao kikosini ni vigumu kupata mbadala, japo tunasubiri hadi dakika ya mwisho kama kuna lolote litatokea tutazungumza."

Nyota huyo amebakiza mkataba wa mwaka mmoja pekee wa kusalia Manchester City na amekuwa akihusishwa kuelekea Saudi Arabia.

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Julai 24-30, 2024 |




# Aziz Ki: Yanga tutaongeza dozi

- Ni baada ya ujio wa mastaa wapya
- Akana kurejeshwa Jangwani na Mlimbwende Hamisa Mobeto




Na Mwandishi Wetu

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Aziz Ki, amesema kuwa, kuongezwa kwa Clatous Chama, Prince Dube, Jean Baleke na Duke Abuya ndani ya kikosi chao kutarahisisha kazi ya kupachika mabao msimu huu unaokuja.

Akiongea kutoka Afrika Kusini, Aziz Ki amepasha kuwa, anaamini msimu ujao watafunga magoli mengi zaidi baada ya kuongezeka kwa wachezaji hao wenye uwezo mkubwa wa kufunga na kuchezesha timu.

"Ni sajili nyingi zimefanyika, lakini nimefurahi kucheza pamoja na Chama, Dube, Abuya na Bareke, ni wachezaji ambao wamekuja kikosini kunipunguzia majukumu hasa eneo la ushambuliaji, msimu ujao nitakuwa na kazi rahisi japo haina maana kwamba nikipata nafasi sitafunga," alisema Aziz Ki na kuongeza.

"Niliposikia Dube anakuja Yanga nilimtabiria ataibuka mfungaji bora, sasa imetimia kazi iliyobaki ni kucheza kwa ushirikiano na kumtengenezea nafasi nyingi za kufunga, kwa upande wa Chama nafikiri kila mchezaji anatamani kucheza naye ni mchezaji ambaye ana uwezo mkubwa wa kuchezesha timu na kutoa pasi za mwisho."

Aziz Ki alisisitiza kuwa amesalia Yanga ili kuendeleza kazi ya kuipambania timu ifikie mafanikio makubwa zaidi na hasa kuvaa medali za Ligi ya Mabingwa baada ya misimu miwili iliyopita kuvaa za Kombe la Shirikisho.

"Maneno yamekuwa mengi kwamba nimebakizwa na mrembo Hamisa Mobeto sio kweli, nimebaki kuipambania Yanga ifikie malengo hilo linawezekana hasa ukiangalia usajili uliofanywa na viongozi kazi imebaki kwetu na benchi la ufundi kuona ni namna gani tunafanya vizuri ndani na nje," alisema Aziz KI.

Nyota huyo aliyekuwa mfungaji bora msimu uliopita kwa mabao yake 21, ametanabahisha kwamba, anatambua ubora wa kila mchezaji aliyepo kikosini na namna kila mmoja anavyotamani kuona wanakuwa bora, hii inanipa morali ya kuamini kuwa msimu ujao tutakuwa bora zaidi," amenena Azizi Ki.

# Kibu Denis azua sitofahamu Simba

Na Valensi Mbaga




WINGA wa Simba SC Kibu Denis Prosper amezua sitofahamu ndani ya klabu hiyo baada ya kushindwa kuripoti kambini huko Ismailia Misri.

Wakati uongozi wa wakisema hawajui mahali alipo Kibu, Meneja wa mchezaji huyo, Sylevester Carlos 'Master Mind' amefichua kuwa, mchezaji huyo yupo Ulaya licha ya kutotaja nchi na kukiri kwamba amelipwa stahiki zake zote na haidai Simba chochote.

Awali Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba SC, Ahmed Ally alisema hana taarifa za nyota huyo kuwa Ulaya na kwamba yeye anachojua Kibu yupo Kigoma huku akiongeza kuwa mwenye nafasi nzuri ya kuzungumzia sababu za Kibu kutokuwepo kambini ni mchezaji mwenyewe.

Baada ya taarifa hiyo Vyanzo vya ndani ya klabu vimethibitisha kuwa Kibu Denis atakatwa nusu ya mshahara wake kimkataba kutokana ana kuchelewa kufika kambini.

Mbali na kukatwa mshahara, chanzo kimedai kuwa sio rahisi kwa Kibu kwenda Misri kipindi hiki na zaidi ataungana na Simba jijini Dar es Salaam itakaporudi.

# BASATA yamfungia Kisauji

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Sanaa la Taifa (BASATA) limemfungia msanii Seif Kassim Kisauji maarufu kama 'Babu TikTok' kutofanya kazi za sanaa ndani na nje ya Tanzania kwa kipindi cha miezi sita kuanzia juzi Julai 22, sambamba na kumtoza faini ya shilingi milioni 3 kwa kutenda kosa la kimaadili wakati akitekeleza kazi zake za sanaa.

Baraza limesema limefikia uamuzi huo baada ya kumuita Kisauji kuhusiana na ukiukwaji wa maadili akiwa kama Msanii aliyesajiliwa na BASATA kwa usajili Na. BST-9684-2023-2154 ambapo ukiukwani huo wa maadili ni kinyume na Kanuni ya 25 (6) ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za mwaka 2018 na Mwongozo wa Uzingatiaji wa Maadili katika Kazi za Sanaa wa Mwaka 2023.

"Baraza la Sanaa la Taifa kupitia Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984 na Maboresho yake ya Mwaka 2019 ina mamlaka ya kusimamia maadili ya msingi kwenye Sekta ya Sanaa kwa Kanuni ya 25(1)-(8) ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2018," imesema taarifa hiyo ya BASATA.

Pia Baraza hilo limesema kuwa, limekwishatoa na kuzindua mwongozo wa maadili katika kazi za sanaa ambao unapatikana katika tovuti yao ya basata.go.tz, hivyo ni jukumu la kila Msanii na Mdau wa Sanaa na jamii kuzingatia maadili katika kazi za sanaa.

